ACT WAZALENDO

2022

MAONI YA ACT WAZALENDO KWA KIKOSI KAZI

CHA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Kuhusu Demokrasia Nchini

MAONI YA ACT WAZALENDO KWA KIKOSI KAZI CHA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KUHUSU DEMOKRASIA NCHINI

1. UTANGULIZI

Misingi ya jamii iliyokusudiwa kujengwa nchini mwetu

Misingi ya Katiba (dibaji/utangulizi) ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania (1977) na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 (RE 2010) inabainisha kuwa ilikusudiwa kujengwa katika nchi yetu jamii inayoongozwa na mambo makuu yafuatayo;

a) **Uhuru**, **haki, udugu na amani (*maridhiano*)**,

b) **Demokrasia** ambayo serikali zake **husimamiwa na Bunge/Baraza la Wawakilishi lenye wabunge na wajumbe waliochaguliwa kidemokrasia na linalowakilisha wananchi (*Tume Huru ya Uchaguzi*)**,

c) **Demokrasia** ambayo serikali zake husimamiwa na **mahakama huru zinazotekeleza wajibu wake wa kutoa haki bila woga** wala upendeleo wowote (***zikizingatia usawa mbele ya sheria***), na

d) Serikali zinazozingatia misingi ya **demokrasia na ujamaa** (***Demokrasia ya vyama vingi na haki za binadamu***)

[maneno yaliyowekewa uzito (bolded) ni kuonyesha **msisitizo]*

Ikizingatiwa taarifa ya Tume ya Jaji Francis Lucas Nyalali (***Nyalali Commission on Multiparty Democracy***) ya mwaka 1991 ambayo ilipendekeza aidha marekebisho au kufutwa sheria 40 ambazo zilionekana kandamizi, kutokana na kukiuka Katiba na kupitwa na wakati kwa;

i. Kunyang'anya uhuru wa wananchi (***freedom***),

ii. Kunyang'anya haki za msingi (***basic rights***),

iii. Kubinya uhuru wa haki za msingi (***impingement of freedom***),

Ni dhahiri marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 2019 yameifanya kuwa miongoni mwa sheria mpya kandamizi nchini mwetu. Mathalani, marekebisho hayo licha ya kumpa mamlaka makubwa Msajili wa Vyama vya Siasa kudhibiti uhuru wa vyama vya siasa (vifungu 12 vyenye adhabu 31), amepewa kinga ya kutoshitakiwa mahakamani jambo ambalo linakinzana na Katiba ya nchi ibara ya (13) juu ya usawa mbele ya sheria.

Katika nchi ambayo inazingatia misingi ya haki, haiyumkiniki kutungwa sheria ambazo kwa taathira ni za kibaguzi. Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania (1977) inatamka ifuatavyo:-

> *“13(1) Watu wote ni sawa mbele ya sheria, na wanayo haki, bila ya ubaguzi wowote, kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria.*
>
> *(2) Ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la* ***ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake.”***

Kama ilivyotafsiriwa na Bingham katika jarida la Cambridge Law Journal, Vol.66, No. 1 (March 2007), pp.67-85, katika makala yake juu ya utawala wa sheria (rule of law), mtu kisheria ni pamoja na mamlaka/idara za serikali. Bingham anasema;

> *"that, all persons and authorities within the state, whether public or private, should be bound by and entitled to benefit of laws publically made, taking effect (generally) in the future and publically administered in the courts."*

Chama cha Siasa

Chama cha siasa ni taasisi ambayo miongoni mwa majukumu yake makuu ni;

a) Kuunganisha watu pamoja (***integration***),
b) Kuunda sera zenye maslahi kwa chama na umma ili kuungwa mkono kwa minajili ya kutimiza malengo yake ya kuongoza serikali (***legitimation***),
c) Kugombea nafasi za uongozi ili kupata uwakilishi (***representation***) na
d) Kuongeza wanachama (***recruitment of political elites***).

Kwa muktadha huo, chama cha siasa hai wakati wote huwa katika harakati kwa ajili ya kuwashawishi na kuwashajihisha (inform and stimulate) wanachama wake na umma kwa ujumla. Pia ni msimamizi (watch dog) wa serikali iliyopo madarakani kwa lengo la kuikosoa na kuishauri kwa kutoa mawazo mbadala. Demokrasia ya vyama vingi inaruhusu ushindani wa sera na mawazo tofauti. Kwa muktadha huo mabadiliko ya madaraka yanapitia ushindani na mchuano mkali wa kisiasa unaotokana na nguvu tofauti kwa sababu ya vyama kujijengea uwezo wa kushindana na kuvumiliana (***capacity to stand up on the opinion of the other).*** Dhana hii inapinga suala la mgombea kupita bila kupingwa.

Mabadiliko ya sheria ya vyama vya siasa ya mwaka 2019 yamefuta uwepo wa vyama vya siasa hai na kujenga himaya ya chama chenye serikali iliyopo madarakani (***one party dominant state***). Aidha vyama vya siasa vinapodhibitiwa kwa kiwango kilichokusudiwa na sheria hiyo (kulingana na maudhui yake), ni dhahiri udhibiti huo unavunja misingi ya Katiba ya kuwa na serikali inayosimamiwa na **mahakama huru inayotoa haki bila upendeleo na Bunge/Baraza la Wawakilishi lenye wabunge na wajumbe waliochaguliwa na linalowakilisha matakwa ya wananchi**, kwani haki mbele

ya sheria (haki ya asili ya kusikilizwa) inatoweka, kanuni za utoaji adhabu (principles of penology) zinakiukwa na wajumbe wa vyombo vya kutunga sheria (wabunge na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi) wanakuwa hawapatikani kwa ridhaa ya wananchi, bali kwa gilba ya chama chenye serikali iliyopo madarakani kwa matumizi ya dola (nguvu ya vyombo vya ulinzi na usalama). Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ni ushahidi tosha juu ya suala hili. Uchaguzi huo ulithibitisha kauli ya aliyekuwa Mwenyekiti wa CCM na Rais wa awamu ya tatu, Hayati Benjamin William Mkapa aliyoitoa mwaka 2005 aliyesema (nukuu);

> *"Duniani kote hakuna hata siku moja utakuta chama tawala kinakubali kushindwa na kuwaachia wapinzani wake watawale.* ***Naahidi kwamba, nitatumia uwezo wangu, nguvu zangu zote na dola kuhakikisha chama chetu (CCM) kinapata ushindi."*** **(msisitizo umeongezwa)**

Kudhibiti shughuli za kisiasa ikiwemo vyama vya siasa, kwa kiwango kilichoasisiwa wakati wa serikali ya awamu ya tano ambapo siasa imejinaishwa (***criminalization of politics***) kwa nia ovu *(**with ulterior and senister motives**)* kumefifisha haki ya kufanya siasa na ni shambulio kwa demokrasia ya vyama vingi na dhana ya uwepo wa vyama huru vya upinzani vinavyowajibika nchini. Aidha ni uuaji wa mafanikio ya demokrasia *(**erode democratic values**)* yaliyofikiwa kwa takriban miaka 27. Hali hiyo imerejesha himaya ya chama kimoja (***one party dominant state***) na utitiri wa vyama vibaraka ***(puppet parties).*** Kwa ujumla wake ni pigo kwa demokrasia na uvunjwaji mkubwa wa Katiba na sheria za nchi (***latest assault on the tenets***).

Aidha ni muhimu kuzingatia kuwa uhuru wa mawazo ni haki ya kikatiba (ibara ya 18), na katika nchi ya kimedokrasia vyama vya siasa ni midomo ya kuwasemea wananchi changamoto zao. Changamoto za wafanyakazi, wakulima, wavuvi, wafanyabiashara, wanahabari n.k. Kutunga sheria za kuwafunga midomo wanasiasa kuzungumzia

changamoto za wananchi ni kupokonya uhuru wa wananchi kutoa maoni na jambo hilo licha ya kuvunja Katiba linakusudia kujenga taifa la majuha kama anavyobainisha Profesa Issa Shivji;

> *"Samaki akifungwa mdomo, anakosa hewa, anakufa kimwili. Binadamu akifungiwa njia za kutoa/kupokea mawazo anakufa kiakili. Inazaa taifa la majuha."*

Lakini pia izingatiwe kuwa, watu wakizuiwa kutoa mawazo yao wanaweza kutafuta namna nyingine ya kusema jambo ambalo ni hatari kwa mustakabali wa umoja na amani nchini (haki, amani na maridhiano).

Kwa kuzingatia hilo, ACT Wazalendo inaona kuwa suluhu ya kweli ya tatizo lililopo ni kufumua mifumo ya uendeshaji wa siasa nchini mwetu na ya uchaguzi ili kuja na mifumo inayoakisi muafaka wa kitaifa. Hata hivyo kwa muktadha wa majukumu ya Kikosi Kazi cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (mabadiliko madogo kuelekea siasa za maridhiano na muafaka wa kitaifa), ACT Wazalendo itatoa maoni na mapendekezo yanayokidhi haja hiyo.

2. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KUFANYIWA KAZI NA KIKOSI KAZI CHA MHESHIMIWA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

A. KATIBA YA JAMHURI YA TANZANIA (1977)

Katiba katika nchi yoyote ya kidemokrasia inapaswa kuwa imetengenezwa kutokana na muafaka wa kitaifa na kwa kuwashirikisha wananchi ambao katika nchi inayofuata mfumo wa jamhuri ***(Republican State)*** ndio wenye nchi ***(Sovereignty belongs to the People).*** Katiba inayotokana na wananchi huwa na uhalali unaotokana na watu ***(legitimacy)*** na wananchi hujiona wana wajibu wa kuiheshimu, kuitii, kuitekeleza, kuilinda na kuitetea. Hali huwa ni tofauti pale Katiba inapoandikwa na kupitishwa na watawala na kuwekwa juu ya wananchi bila ya ushiriki wao katika kuitengeneza.

Kwa hatua tuliyofikia, mahitaji ya Katiba Mpya sio suala la kubishaniwa tena. Kama Taifa tulishakubaliana kuhusu haja na hoja ya kuandika Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo itatokana na ushiriki wa Watanzania wenyewe na itafsiri matakwa ya Watanzania na kubeba matumaini na matarajio yao kulingana na zama za sasa na zijazo.

Hakuna asiyefahamu historia ya kikatiba ya nchi zetu mbili zinazounda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katiba ya Tanganyika ya mwaka 1961 ilitengenezwa na Waingereza kwa ushiriki mdogo sana wa wanasiasa wa Chama cha TANU kwa malengo ya kutumika baada ya Uhuru wa Tanganyika. Katiba hiyo ilimtambua Malkia wa Uingereza kama mkuu wa nchi ya Tanganyika na ilitambua uwepo wa Gavana wa Kiingereza aliyemwakilisha Malkia huyo. Katika Katiba hiyo, Waziri Mkuu wa Tanganyika hakuwa na uamuzi wa mwisho katika mambo mengi ya uendeshaji wa nchi na badala yake alilazimika kushauriana na kuafikiana na Gavana wa Kiingereza katika uamuzi huo.

Katiba ya Jamhuri ya Tanganyika ya mwaka 1962 nayo ilitungwa na Bunge la Tanganyika lililokuwa limehodhiwa

na TANU na kwa msukumo mkubwa wa Serikali ya TANU iliyokuwepo madarakani na zaidi ilibeba maono ya mtu mmoja, yaani Mwalimu Julius Nyerere. Utungaji wa Katiba hiyo haukuwashirikisha wananchi. Katiba ya 1962 ndiyo iliyokuja na dhana ya Urais wa Kifalme ***(Imperial Presidency)*** ikiwa imelimbikiza madaraka makubwa kwa Rais.

Katiba ya Muda (Interim Constitution) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 1964 kimsingi ilikuwa ni Katiba ileile ya Jamhuri ya Tanganyika ikiwa imefanyiwa marekebisho ili kuifanya iweze kukidhi matakwa ya Muungano. Nayo utungaji wake haukushirikisha wananchi. Kwa mujibu wa Mkataba wa Muungano (Articles of Union), Katiba hii ilikusudiwa itumike kwa mwaka mmoja mpaka pale itakapotungwa Katiba ya Kudumu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ambayo ilipaswa iwe imetungwa sio zaidi ya tarehe 25 Aprili, 1965 lakini hilo halikufanyika.

Katiba ya pili ya Muda (Interim Constitution) ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1965 nayo ilipitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano likiwa na wabunge wa TANU na wabunge wachache walioteuliwa kutoka Zanzibar. Katiba hii iliweka msingi wa TANU kushika hatamu na iliingiza Katiba ya TANU kama sehemu ya Katiba ya Muungano ikiwa ni Nyongeza (Schedule) kwenye Katiba hiyo. Katiba hii ya pili ya Muda nayo haikutungwa kwa kushirikisha wananchi na iliendelea kufanyiwa marekebisho makubwa hadi mwaka 1977 kutegemeana zaidi na utashi wa TANU na Rais wa Jamhuri ya Muungano ambaye pia alikuwa Rais wa TANU.

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambayo ndiyo inayoendelea kutumika hadi sasa ni Katiba iliyotungwa kupitia kamati ya wajumbe 20 kutoka vyama vya TANU na ASP ambayo ni kamati iliyosimamia kuunganisha vyama hivyo kuunda Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kutayarisha Katiba ya CCM. Mapendekezo ya kamati hiyo yalipelekwa Bungeni ambako yalipitishwa

ndani ya muda wa saa chache. Hakukuwa hata na mjadala wa maana. Katiba ya mwaka 1977 nayo iliandikwa bila kushirikisha wananchi.

Mwaka 1992, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliingia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa. Tume ya Rais iliyokuwa chini ya Jaji Mkuu wa wakati huo, Francis Nyalali ilipewa kazi ya kukusanya maoni ya wananchi iwapo wangependa Tanzania ibaki kuwa nchi ya chama kimoja cha siasa au iruhusu mfumo wa vyama vingi vya siasa. Katika kukusanya maoni hayo, Tume hiyo ilisema asilimia 80 ya waliotoa maoni walitaka nchi iendelee kuwa ya chama kimoja huku asilimia 20 wakitaka mfumo wa vyama vingi uruhusiwe. Kwa upande wa Zanzibar, Tume hiyo ilisema asilimia 56 ya waliotoa maoni walitaka mfumo wa chama kimoja uendelee na asilimia 44 walitaka mfumo wa vyama vingi uruhusiwe. Hata hivyo, Tume hiyo ilibaini kwamba hata waliopendekeza mfumo wa chama kimoja walitaka marekebisho makubwa ambayo kwa maoni ya Tume isingewezekana kufanyika ndani ya mfumo wa chama kimoja; na hiyo ikawa ndiyo sababu ya Tume hiyo kupendekeza mabadiliko ya mfumo wa siasa kuruhusu mfumo wa vyama vingi.

Pamoja na mambo mengine, Tume hiyo ilipendekeza kuandikwa kwa **KATIBA MPYA** ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuendana na matakwa na mahitaji ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi. Tume hiyo ilipendekeza iundwe Tume ya Katiba (Constitutional Commission) na kisha kuundwe chombo ambacho tungekuwa kama Mkutano wa Katiba (Constitutional Conference) utakaokuwa na uwakilishi mpana wa makundi mbalimbali **katika** nchi ili kujadili mapendekezo yatakayotolewa na Tume ya Katiba na kisha kupitisha Katiba Mpya.

Tume ya Nyalali pia ilipendekeza mambo kadhaa ambayo tunaweza kusema misingi yake ilipaswa izingatiwe katika Katiba Mpya itakayotungwa. Miongoni mwa mambo hayo ni:

1. Kufutwa au kurekebishwa kwa sheria 40 kandamizi ambazo misingi yake haikubaliki katika nchi inayofuata demokrasia ya vyama vingi na inayozingatia na kuheshimu haki za binadamu na utawala wa sheria;

2. Kuunda upya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) ili kuzifanya kuwa **TUME HURU ZA UCHAGUZI**;

3. Kuandika upya au kufanya marekebisho makubwa ya Sheria ya Uchaguzi ya Taifa (National Elections Act) na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar (Zanzibar Elections Act) ili kuzifanya zizingatie matakwa na misingi ya demokrasia ya vyama vingi;

4. Vyombo vya Ulinzi na Usalama (JWTZ, Usalama wa Taifa, Polisi, Jeshi la Kujenga Taifa na Idara Maalum za SMZ) kufanyiwa marekebisho makubwa ili kuvitoa katika siasa na kujiegemeza kwenye CCM kwa kuzingatia kuwa upatikanaji wake ulikuwa umefungamanishwa na chama hicho kilichokuwa pakee yake;

5. Marekebisho makubwa ya mfumo na muundo wa utawala (Administrative Structure and System) katika ngazi za mikoa, wilaya, tarafa na kata/wadi ili kuondoa utaratibu uliorithiwa ambao ulikuwa umehodhiwa na chama kimoja na kuwa na mfumo wa kidemokrasia utakaoweka misingi bora na imara ya uwajibikaji;

6. Mali zote zinazomilikiwa na CCM zilizotokana na michango ya wananchi wote wakiwemo ambao hawakuwa wanachama wala wafuasi wa chama hicho ambazo ni pamoja na majengo, viwanja vya michezo na ardhi zirudishwe Serikalini kwani sio halali kuendelea kumilikiwa na CCM wakati zilitokana na michango ya Watanzania wote;

7. Kuwa na kipindi cha mpito cha miaka miwili kuruhusu marekebisho hayo kufanyika kabla ya kuitishwa kwa Uchaguzi Mkuu wa 1995.

Bahati mbaya, Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambacho ndicho kilijipa mamlaka ya kusimamia mabadiliko yaliyopendekezwa kutoka mfumo wa chama kimoja kwenda demokrasia ya vyama vingi, kupitia Mkutano Mkuu wake wa Taifa uliofanyika Februari 1992, kiliyakataa mengi kati ya mapendekezo hayo. Badala yake, kiliamua yafanyike machache ya Katiba ya mwaka 1977 iliyopo na baadhi ya sheria ili kuruhusu mfumo wa vyama vingi uanze huku mfumo mzima wa kikatiba, kisheria, kiuchaguzi, kiutawala na kiulinzi ukibaki kuwa uleule uliowekwa ili kukilinda, kukihami na kukitumikia chama kimoja - CCM.

Ni kutokana na hali hiyo ndiyo maana Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla na Zanzibar kwa namna ya pekee zimejikuta zikitumbukia katika migogoro kila wakati wa uchaguzi na hata baada ya uchaguzi, migogoro ambayo imechangia hadi watu kuuawa, kuumizwa, kujeruhiwa, na wakati mwingine kuzalisha wakimbizi wa kisiasa kama ilivyotokea mwaka 2001 na mwaka 2020.

Katika hali hii, hatuwezi kukwepa hoja na haja ya kuandikwa **KATIBA MPYA** itakayotokana na maoni ya wananchi na ambayo itakidhi mahitaji ya mfumo wa demokrasia ya vyama vingi. Bahati nzuri tayari kazi hiyo ilishaanza. Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (***Constitutional Review Act***) na Sheria ya Kura ya Maoni ***(Referendum Act)*** zilipitishwa, Tume ya Mabadiliko ya Katiba ikaundwa chini ya Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba ikakusanya maoni ya Watanzania na hatimaye ikatoa Rasimu ya Awali na kisha Rasimu ya Pili ya Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Bahati mbaya ni kwamba Bunge Maalumu la Katiba lilishindwa kujenga muafaka wa kitaifa na kazi ya kupitisha Katiba Mpya ikachukua sura ya mivutano na malumbano

makali ya kisiasa baina ya kambi mbili zinazopingana. Hatimaye, kambi moja ikaamua kususia Bunge la Katiba na matokeo yake Katiba Inayopendekezwa iliyokuja kupitishwa haikuwa tena na sura ya Katiba iliyobeba muafaka wa kitaifa. Nchi ikajikuta katika mkwamo ambao umeligawa Taifa letu. Kazi inayotukabili sasa ni kuona vipi tutatoka katika mkwamo huo.

KWA NINI KATIBA INAYOPENDEKEZWA HAINA SIFA YA KUWA KATIBA MPYA YENYE KUBEBA MUAFAKA WA KITAIFA?

Kuna hoja na dhana inajengwa na baadhi ya wanasiasa hususan wale wa chama tawala kwamba iwapo mchakato wa Katiba Mpya uendelee, basi unapaswa kuendelezwa kwa kupeleka **Katiba Inayopendekezwa** kwa wananchi ili kupigiwa kura ya maoni na kuanza kutumika. Sisi katika ACT Wazalendo hatukubaliani na hoja hiyo kwa sababu Katiba Inayopendekezwa ilipitishwa kwa hila na ujanja na upande mmoja, na haikutokana na muafaka wa kitaifa ambao ndiyo unapaswa kuwa msingi wa Katiba Mpya.

Hoja yetu ni kwamba Katiba Inayopendekezwa ilitengenezwa na CCM kupitia vikao vyake na ikapenyezwa vipande vipande katika Bunge Maalumu la Katiba kupitia wajumbe wa chama hicho bila kuzingatia matakwa ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba kazi ya kutafsiri maoni ya wananchi na kutengeneza Rasimu ya Katiba ilitolewa kwa chombo kimoja tu ambacho ni Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyokuwa ikiongozwa na Jaji Joseph Sinde Warioba. Tume hiyo ilifanya kazi hiyo na kutoa Rasimu ya Awali na kisha Rasimu ya Mwisho ya Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo iliwasilishwa mbele ya Bunge Maalumu la Katiba kwa ajili ya kuiweka sawa (refine) na kisha kuipitisha. Sheria ya Mabadiliko ya Katiba haikutoa fursa kwa chombo kingine (na kwa hapa tunazungumzia CCM iliyotengeneza rasimu yake na kuipenyeza kwenye Bunge Maalumu la Katiba) kubadilisha maoni ya wananchi.

Kwa mujibu wa baadhi ya waliokuwa wajumbe wa Kamati ya Uandishi ya Bunge Maalumu la Katiba, CCM ilitengeneza kikosi chake kilichoundwa na Andrew Chenge, Dk Asha Rose Migiro na Profesa Costa Ricky Mahalu na wakaandaa rasimu yao ambayo ndiyo iliyopenyezwa kwenye Bunge Maalumu la Katiba na kuchakachua pamoja na kubadilisha maoni ya wananchi waliyoyatoa mbele ya Tume ya Jaji Warioba.

Mbali na hoja hizo, Katiba Inayopendekezwa haiwezi kukubalika Zanzibar kwa sababu inaifanya Zanzibar kuwa kama ni serikali ya jimbo au manispaa (Municipal Government). **Hilo halitakubalika kwa namna yoyote ile kwa Wazanzibari**.

Kutokana na hoja hizo, sehemu ya kuanzia katika kuipata Katiba Mpya ni kurudi kwenye Rasimu ya Katiba Mpya iliyotokana na maoni ya wananchi kama yalivyotafsiriwa na kuratibiwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyoongozwa na Jaji Joseph Sinde Warioba

Mapendekezo ya ACT Wazalendo kufanikisha eneo hili ni kama ifuatavyo:

- Mchakato wa Katiba Mpya uanzishwe mara moja sambamba na hatua za kufanya mabadiliko ya msingi (minimum reforms) yatakayokidhi mahitaji ya muda mfupi na muda wa kati kuelekea Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji wa 2024 na Uchaguzi Mkuu wa 2025. Mchakato wa kupata Katiba Mpya unaweza kuanzishwa tena kati ya Oktoba 2022 hadi Agosti 2024 na kuona hatua itakayofikiwa (kulingana na mapendekezo yetu yanayofuata hapa chini). Iwapo mchakato huo utakamilika na kutupatia Katiba Mpya katika kipindi hicho litakuwa jambo jema. Lakini iwapo mchakato huo hautakamilika ifikapo Agosti 2024, basi usimamishwe katika hatua itakayokuwa imefikiwa katika muda huo na kuendelezwa tena mara tu baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2025 hadi kukamilika

kwake. Ili kuipa Katiba Mpya uhalali unaotokana na watu ***(legitimacy)*** na wananchi kujiona wana wajibu wa kuiheshimu, kuitii, kuitekeleza, kuilinda na kuitetea tunapendekeza mchakato uanzie katika **Rasimu ya Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba**. Rasimu Pendekezwa iliyotokana na Bunge la Katiba baada ya kumeguka sehemu mbili, haina uhalali kutokana na mchakato kuporwa kwa itikadi za kisiasa. Kimsingi inaifanya Zanzibar kuwa kama Manispaa ya Mji wa Tanzania Bara na hivyo haiwezi kukubalika kupitia kura ya maoni ***(Referendum).***

1. Hatua ya mwanzo tunayopendekeza ifanyike ni kupitiwa upya na kufanya marekebisho/mabadiliko ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba **(Constitutional Review Act)** na Sheria ya Kura ya Maoni **(Referendum Act)** ili kukidhi matakwa ya sasa ya muda (tarehe zilizoainishwa mle zimeshapitwa na wakati), kuamua mchakato wa kupata Katiba Mpya uendelezwe kuanzia hatua ipi, na pia kutambua maeneo yaliyosababisha mkwamo katika mchakato wa 2011 – 2014 na kuyafanyia marekebisho ili kuepuka mkwamo mwingine (ikiwemo muundo wa wajumbe wa Bunge la Katiba au kama kuna haja ya kuja na mfumo mwengine wa chombo kingine cha kupitisha Katiba Mpya na namna ya kusuluhisha tofauti kubwa zinapojitokeza miongoni mwa wajumbe). Tunapendekeza kuitisha Mkutano wa Majadiliano ya Kitaifa ***(National Consultative Conference)*** utakaojumuisha Serikali, vyama vya siasa, asasi za kiraia, asasi za kidini, wasomi wabobezi wa sheria hasa katika maeneo ya Katiba na Utawala (Constitutional and Administrative Law), na makundi mbalimbali ya kijamii ili kukubaliana juu ya marekebisho/mabadiliko ya sheria hizo mbili na namna ya kuuendea mchakato mzima wa kupata Katiba Mpya. Makubaliano ya mkutano huo ndiyo yaongoze utayarishaji wa miswada ya sheria ya

marekebisho/mabadiliko ya sheria hizo itakayowasilishwa Bungeni kwa ajili ya kupitishwa.

2. Hatua ya pili tunayopendekeza iwe ni kujenga muafaka wa kitaifa kuhusiana na maeneo makubwa na muhimu yanayogusa mfumo wa kikatiba wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo yamekuwa ndio chanzo na sababu ya mivutano katika maudhui ya Katiba Mpya. Maeneo hayo ni pamoja na ***Muungano na muundo wake, madaraka ya Rais, mgawanyo wa madaraka kati ya Bunge (Legislature), Serikali (Executive) na Mahakama (Judiciary*) na mfumo wa uchaguzi na uendeshaji wake.** Tunapendekeza utaratibu uleule wa kuwa na Mkutano wa Majadiliano ya Kitaifa ***(National Consultative Conference)*** utakaojumuisha Serikali, vyama vya siasa, asasi za kiraia, asasi za kidini, wasomi wabobezi wa sheria hasa katika maeneo ya Katiba na Utawala (Constitutional and Administrative Law), na makundi mbalimbali ya kijamii utumike katika hatua hii kujenga na kupata muafaka wa kitaifa kuhusiana na maudhui ya Katiba Mpya. Muafaka wa kitaifa ukishajengwa katika hatua hii na kukubaliwa kwa dhati, kazi ya kupitisha Katiba Mpya katika chombo chochote kitakachopewa dhamana hiyo itakuwa sio ngumu.

3. Hatua ya tatu tunayopendekeza itakuwa ni kuunda Timu ya Wataalamu Wabobezi ***(Constitutional Experts Commission),*** kutoka ndani na nje ya nchi kadiri itakavyoonekana inafaa ambao watayaweka yaliyokubaliwa kwenyem muafaka wa kitaifa kupitia Mkutano wa Majadiliano ya Kitaifa (National Consultative Conference) tulioutaja kwenye kifungu nambari 2 hapo juu katika Rasimu ya Katiba (Draft Constitution). Ifahamike hapa kuwa rasimu inayozungumziwa ni ile ya **Jaji Mstaafu Joseph Sinde Warioba.** Rasimu hiyo ya Katiba itawasilishwa kwenye chombo kitakachopewa

dhamana ya kutunga Katiba Mpya ***(Enactment of the new Constitution)*** kama ilivyokubaliwa kwenye Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (rejea maelezo ya kifungu nambari 2 hapo juu) kwa ajili ya kupitishwa.

4. Hatua ya nne ni Katiba Mpya kufikishwa kwa wananchi kwa ajili ya kupigiwa **KURA YA MAONI *(referendum)*** ambapo iwapo itaungwa mkono na wananchi wengi (simple majority) wa upande wa Tanganyika na wananchi wengi (simple majority) wa upande wa Zanzibar, basi itakuwa imeridhiwa na kuidhinishwa rasmi.

5. Iwapo katika hatua yoyote kutajitokeza mkwamo au kutokubaliana, tunapendekeza kuwa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba izingatie namna ya kukwamua au kusuluhisha mkwamo au tofauti hizo kwa namna kama ile tulioitaja kwenye kifungu nambari 1 hapo juu kuhusiana na tofauti zinazoweza kujitokeza katika chombo chochote kitakachopewa dhamana au Bunge Maalumu la Katiba (endapo itaamuliwa liendelee kuwepo).

B. MFUMO WA MARIDHIANO ILI KUDUMISHA HAKI, AMANI NA UMOJA WA KITAIFA

Historia ya kisiasa ya Tanzania imeacha majeraha na makovu mengi tangu kurudishwa tena kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992. Kwa muda mrefu, hali hiyo ilionekana Zanzibar lakini katika kipindi cha miaka sita iliyopita (2015 – 2021) hali pia ilitetereka Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar yapo pia majeraha na makovu yanayotokana na harakati za kisiasa wakati wa kupigania Uhuru. Panahitajika njia ya kutibu majeraha na makovu haya ili kuzifanya nchi zetu zisonge mbele.

Zanzibar ina uzoefu fulani kuhusiana na muafaka na maridhiano katika vipindi mbalimbali ambayo yamesaidia kutuliza hali kwa kiasi fulani. Hata hivyo, bado kumejitokeza changamoto kubwa kama ilivyoonekana miaka ya 2015 – 2020.

Njia pekee ambayo sisi ACT Wazalendo tunaiona inaweza kutibu majeraha na makovu haya na kupata maridhiano ya kitaifa ili kudumisha haki, amani, utulivu na umoja wa kitaifa ni mazungumzo baina ya makundi mbalimbali hapa nchini na hasa vyama vya siasa na Serikali. Lililo la muhimu ni kuwa na **DHAMIRA YA DHATI (utashi wa kisiasa)** ya kupata **MARIDHIANO YA KWELI**.

Tunapendekeza kwamba kuwepo na **JUKWAA LA KUDUMU LA MAJADILIANO** litakalohusisha vyama vya siasa na wahusika wengine muhimu ikiwemo Serikali. Kwa mtazamo wetu Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD) kinaweza kufanya kazi hii. Tunapendekeza kutumia uzoefu wa Zanzibar wa mwaka 2002 - 2005 ambapo ilianzishwa **Tume ya Rais ya Pamoja ya Usimamizi (Joint Presidential Supervisory Commission - JPSC)** kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Wawakilishi na hivyo kufanya kazi zake ziwe na nguvu za kisheria. TCD (**Tanzania Center for Democracy**) inaweza ikaanzishwa rasmi sasa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge na kuangaliwa

namna bora ya kuimarisha muundo wake ili iwe ndiyo Jukwaa la Kudumu la Majadiliano.

Kupitia jukwaa hilo, mambo yote yanayokwaza haki, amani, utulivu na umoja wa kitaifa yanaweza kuwasilishwa na kujadiliwa kwa lengo la kupata ufumbuzi wa pamoja.

Kunaweza pia kukawa na mkutano wa kila mwaka (Annual Conference) wa TCD (kama itakavyorekebishwa kupitia Sheria ya Bunge) utakaowahusisha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar ili kutoa fursa ya kuwa na mjadala wa kitaifa wa mambo ya msingi yanayohusu uendelezaji na uimarishaji wa haki, demokrasia, amani, utulivu na umoja wa kitaifa.

Katika kupata muafaka wa kitaifa katika mambo muhimu yanayogusa masuala ya haki, demokrasia, amani, utulivu na umoja wa kitaifa, Serikali inaweza kupeleka mapendekezo ya miswada ya sheria au hatua nyingine inazokusudia kutekeleza mbele ya TCD ili kupata maoni ya wahusika na hivyo kupunguza misuguano na kujenga utamaduni mpya wa kisiasa hapa nchini.

Kwa upande mwingine ili kuyatibu maumivu, majeraha na makovu yaliyotokana na vitendo vya uvunjaji wa haki za binadamu tangu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa hapa nchini, ACT Wazalendo tunapendekeza kuanzisha **Tume ya Haki, Ukweli na Maridhiano (Justice, Truth and Reconciliation Commission)** itakayotoa nafasi ya kuwasikiliza waathirika wa vitendo hivyo na pia wanaotuhumiwa kutenda vitendo hivyo na kupendekeza hatua za kuchukuliwa ili kuliponya Taifa

C. MIKUTANO YA HADHARA NA MIKUTANO YA NDANI YA VYAMA VYA SIASA

Kimsingi sheria ya vyama vya siasa kama ilivyofanyiwa marekebisho makubwa mwaka 2019 inahitaji kufutwa na kutungwa upya. Hata hivyo bila kuathiri yaliyomo kwenye utangulizi, na kwa minajili ya kuifanyia marekebisho madogo ili iweze kukidhi haja ya uwepo wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa katika muda huu mfupi, ACT Wazalendo inapendekeza marekebisho yafuatayo:

1) Kufutwa kwa kifungu 11(2) kinachotoa mamlaka ya matumizi ya vifungu vya 43 – 46 vya sheria ya Jeshi la Polisi (Police Force and Auxilliary Service Act Cap 322 of 1973) katika mchakato wa uitishwaji wa mikutano ya vyama vya siasa. Kwa maudhui ya vifungu 43 – 46 vya Sheria ya Jeshi la Polisi, taarifa kwa Jeshi la Polisi inatafsirika kana kwamba ni kuomba kibali na kama kibali hakijatolewa basi kwa utashi wa Jeshi la polisi wakati wowote mkutano unaweza kuvunjwa hata kama utakuwa umeanza na unaendelea. Vilevile pamoja na kwamba taarifa ni kwa ajili ya mikutano ya hadhara, Jeshi la Polisi kwa utashi wake limekuwa likitumia kifungu hiki kuingilia vikao/mikutano ya ndani ya vyama vya siasa vya upinzani kwa kuiita mikusanyiko haramu. Hayo ndiyo yamekuwa mazoea hususan katika kipindi cha miaka sita (6) ya serikali ya awamu ya tano.

   Mapendekezo ya ACT Wazalendo ni kukiandika upya kifungu cha 11(2) ili kisomeke ifuatavyo:

   > *11(2)(a) Nothing in section 11(1)(a) shall be construed as applying for permission from the police officer inchage to hold meetings, but a notification for the protection and assistance of the security agencies for the purposes of facilitating peaceful and orderly meetings.*

(b) No notification shall be given to the police officer in charge of any area concerned for purposes of holding party internal meetings;

Ifahamike kuwa vifungu 43 – 46 vya Jeshi la Polisi vilitungwa kukidhi mahitaji ya mikutano na mikusanyiko mingine (maandamano, mikutano ya kidini, mikutano ya wafanyakazi n.k.) kwani wakati huo (1973) nchi ilikuwa na chama kimoja cha siasa na hivyo Jeshi la Polisi halikuhusika kabisa na mikutano ya kisiasa. Sheria ya vyama vya siasa (mwaka 1992 Toleo la 2019) imevipa haki vyama vya siasa kufanya mikutano kwa kutoa taarifa Polisi ili kupata ulinzi. Haiwezekani sheria ya vyama vya siasa ikatoa haki halafu ndani yake kukawa na vifungu *(**clause potestative/exlegare;*** which means to deprive one of the benefit and protection of the law) vinavyoondoa haki hiyo.

2) Vilevile kukifanyia marekebisho kifungu cha 11(8) kutoa muda ambao ndani yake ofisa wa Jeshi la Polisi aliyepewa taarifa ya mkutano wa chama cha siasa atapaswa kujibu kuzuia mkutano usifanyike kama kuna sababu za msingi kufanya hivyo. Kifungu hicho kisomeke ifuatavyo:

*11(8) A stop order referred to under subsection (6) shall be made in writing **within 12 hours after reception of a notification from a Political Party,** and in such form as is able to easily disclose the reasons for its issuance and state whether or not the political party concerned may hold the meeting or procession at the venue or place at another time or date convenient to it in the same area and shall not be given except for the reasons described here under:-*

a) Coincidence of two party meetings in tha same area and time,

b) Coincidence of the public meeting and government/Community programmed activity,
c) State of emergency.

Kujibiwa ndani ya saa 12 kunalenga kukifanya chama kilichotoa taarifa kutoendelea na maandalizi na hivyo kukiepusha kuingia gharama.

3) Kifungu cha 8E kinachohusu makundi ya ulinzi kwa vyama vya siasa kifutwe na kiandikwe upya kuzingatia uamuzi wa Mahakama ya Afrika Mashariki ambayo ilitamka kuwa kinakinzana na mkataba wa Afrika Mashariki ambao Tanzania ni mwanachama na imeuridhia. Kifungu hicho inapendekezwa kisomeka ifuatavyo:

> *8E. – A political party, a leader or member shall not recruit, deploy or form a militia or paramilitary* ***except party members security groups meant to facilitate protection to its leadres and maintain security to the party properties.***

D. RUZUKU KWA VYAMA VYA SIASA

Sehenu ya V inayohusu fedha kwa vyama vya siasa (**Funds and other resources of a party)**

1) Kifungu cha 16(1) kiboreshwe kwa kuongezewa **sharti** (the subvention provision to be fenced) la tengo la ruzuku kwa vyama vya siasa kuwa kati ya asilimia moja na mbili ya bajeti ya mwaka wa serikali na kisomeke ifuatavyo:

> *16(1) The Government shall, subject to section 17, disburse up to **not less than one per centum** and not more than two per centum of the annual recurrent budget less the amount payable in defraying the national debt in the grant of subventions to political parties in pursuance of the provisions of this Act.*

Maboresho hayo yanalenga kulinda lengo la ruzuku kwa vyama vya siasa kwani bila kufanya hivyo, serikali inaweza kutenga asiliomia tatu (0.3%) ya bajeti yake kiwango ambacho ni pungufu ya asilimia mbili (2%).

2) Kifungu cha 16(3) kinachoainisha sifa za chama kustahiki ruzuku kiboreshwe kwa kuongeza fasili mpya tano (5) zinazoshajihisha vyama vyote vya siasa kushiriki uchaguzi, kuzingatia uwiano wa jinsia na kuwa na matumizi mazuri ya fedha za umma zitakazotolewa kama ruzuku. Kifungu hicho inapendekezwa kisomeke ifuatavyo: -

> *"16(3) No party shall qualify for the grant to it of a subvention in accordance with this Act unless: -*
>
> *(a) It is a party which is fully registered and maintains conditions* prescribed for full registration *under this Act,*

(b) Has been inspected by the Registrar of political parties,

(c) It has put up not less than 5% of its candidates in the immediately preceding Civic Elections,

(b) It has, in the immediately preceding general and local government election, had any of its candidates elected to be a Member of Parliament or member of a local government authority,

(d) *It has, participated in the immediately preceding general election and has attained at least 3% of the total valid votes for parliamentarians.*

(e) *It has, participated in the immediately preceding general election and has attained at least 1% of the total valid votes for councillors.*

(f) Not less than 30% of its national leaders are women,

(g) It has not attained either adverse or disclaimer opinion from the immediately preceding financial statements audited by the Controller and Auditor General.

3) Kifungu cha 17(2) kinachohusu mgawo wa ruzuku kiboreshwe kuwezesha vyama vyote vyenye usajili wa kudumu na vinavyokidhi matakwa ya kifungu cha 16(3) kupata ruzuku ya serikali. Kifungu hicho inapendekezwa kisomeke ifuatavyo:

*2(a) **ten** per centum of the funds shall be disbursed equally amongst qualifying parties on the basis of the conditions prescribed in sec. 16(3),*

*(b) **forty** per centum of the funds shall be disbursed amongst qualifying parties on basis of the ratio of parliamentary seats;*

***(c) Twenty-five** per centum of the funds shall be disbursed amongst qualifying parties on basis of the ratio of parliamentary valid votes*

*(c) **Twenty-five** per centum of the funds shall be disbursed amongst qualifying parties based on ratio of the councillors valid votes.*

4) Kufuta kifungu cha 16(2) kwani marekebisho yaloyofanywa katika kifungu cha 17(2)(c) yamezingalia maudhui ya kifungu hicho.

5) Kufutwa kwa kifungu cha 17(3) kwa sababu ya kukinzana na ibara za 66(1)(a) na 77(1) zikisomeka kwa pamoja. Kwa maudhui ibara hizo zinakataa mgombea kupita bila kupingwa. Aidha kifungu hicho kikibakia kama kilivyo kitakuwa kinayafanya mapendekezo ya ACT Wazalendo katika vifungu 16(3) na 17(2) kukosa maana.

E. MASUALA YANAYOHUSU UCHAGUZI

(a) Uchaguzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Kwa muktadha wa kazi ya Kikosi Kazi cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, maoni yetu katika muda mfupi ni marekebisho madogo yafuatayo:

1. **Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)**

1) Katiba ya nchi katika ibara ya 74(1) iongezwe **maneno "TUME HURU YA UCHAGUZI''** na ambayo ndiyo itasimamia uchaguzi wowote nchini na jinsi wajumbe wake watakavyopatikana.

Ibara hiyo isomeke ifuatavyo:

*74.-(1) Kutakuwa na **Tume Huru ya Uchaguzi** ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **ambayo itasimamia uchaguzi wa Rais, Wabunge, Madiwani na Wajumbe wa Serikali za Mitaa** ambayo itakuwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wengine watano (5) watakaoteuliwa na Rais kutokana na mapendekezo ya **Kamati Maalumu ya Uteuzi*** (selection panel) *itakayokuwa na wajumbe wafuatao:*

Kamati ya Uteuzi itakuwa na wajumbe saba (7) wafuatao:-

a) Wajumbe wawili kutoka majaji wa Mahakama ya Rufaa au Mahakama Kuu ya Tanzania watakaopendekezwa na Tume ya Utumishi ya Mahakama kwa kuzingatia jinsia na kukubaliwa na vyama vya siasa vyenye uwakilishi kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

b) *Wajumbe wawili kutoka asasi za kitaifa za masuala ya sheria na haki za binadamu watakaopendekewa na asasi hizo na kukubaliwa na vyama vya siasa vyenye uwakilishi kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,*

c) *Wajumbe wawili kutoka Chama cha Wanasheria Tanzania (Tanganyika Law Society) watakaopendekezwa na chama hicho (kwa kuzingatia jinsia) na kukubaliwa na vyama vya siasa vyenye uwakilishi kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

d) *Mjumbe mmoja kutoka Chama cha Wanasheria Wanawake atakayependekezwa na chama hicho na kukubaliwa na vyama vya siasa vyenye uwakilishi kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

2) Kuifuta na kuiandika upya ibara ndogo ya 74(5) ya Katiba kwani baada ya marekebisho ya ibara ya 74(1) itakuwa haina maana (superfluous). Ibara mpya 74(5) inapendekezwa kusomeka ifuatavyo:

> *75(5) Madaraka ya kudhibiti nidhamu ya watu hao na madaraka ya kuwaondoa kazini yatakuwa mikononi mwa Kamati Maalumu ya Uteuzi iliyotajwa katika ibara ndogo ya (1) ya ibara hii kwa utaratibu ule ule wa kuwandoa majaji wa Mahakama Kuu madarakani.*

Imani yetu ni kuwa ikitamkwa bayana ni **HURU**, wajumbe wake kuteuliwa na masuala ya nidhamu yao kupitia Kamati Maalumu ya Uteuzi, basi suala la kufanya kazi kwa mashaka, woga na kulazimishwa

kupokea maelekezo kutoka kwa aliyewateua yatapungua. Pia masharti ya ibara za 74(7) na 74(11) yatakuwa na mantiki.

3) Kufanya marekebisho ya Ibara ya 74(6) (a & b) vizomeke ifuatavyo:

74(6) Majukumu ya Tume Huru ya Uchaguzi yatakuwa ni:

(a) Kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura katika uchaguzi wa Rais, wabunge, ***madiwani na viongozi wa Serikali za mitaa*** *katika Jamhuri ya Muungano;*

(b) kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uchaguzi wa wa Rais, wabunge, ***madiwani na viongozi wa Serikali za mitaa****;*

2. Kufuta vifungu vilivyoainishwa katika sheria kadhaa na kuviandika upya visomeke ifuatavyo:

1) Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura 343:

a) 7(1) There shall be Returning and Assistant Returning Officers appointed by ***the Independet Electoral Commission*** *for the purpose of conducting an election in each and every electoral constituency, ward, village and harmlets.*

b) 7(2) Every Returning Officer and Assistant Returning Officer shall before be embarking on the functions of that office during any elections, take an oath of secrecy in the prescribed form before a magistrate.

c) *7A(1)There shall be Registration and Assistant Registration Officers appointed by the Independet Electoral Commission for the purpose of registration of voters in each and every electoral constituency.*

d) *7A(2) Every Registration and Assistant Registration Officers shall before embarking on the functions of that office during any elections, take an oath of secrecy in the prescribed form before a magistrate.*

Lengo la marekebisho haya ni kuwaodoa wakurugenzi wa halmashauri za wilaya na maafisa watendaji wa kata na vijiji kusimamia uchaguzi ili Tume iajiri wafanyakazi wake yenyewe.

e) Kifungu cha 38A(2) kuhusiana na dhamana ya fedha ya mgombea aliyepita bila kupingwa (jambo linalokinzana na ibara ya 66 ya Katiba ya nchi (wabunge wa majimbo ni wa kuchaguliwa) kifutwe na kuandikwa upya kisomeke ifuatavyo:

> *38A(2) The deposit of nominated candidate shall be forfeited to the Government if he withdraws his candidature after nomination day or if the number of votes counted in his favour at the election, is less than one-tenth of the total number of votes counted for the constituency for which he was a candidate, except that such deposit shall not be forfeited if the candidate dies.*

f) Kifungu cha kupita bila kupingwa kifutwe na kuandikwa upya ili kuondoa dhana ya mgombea kupita bila kupingwa na kisomeke ifuatavyo:

> *44. Where on the date and time appointed for the purpose of submission of the names of the candidates, only the name of one candidate is validly submitted, the Independent Electoral Commission shall nominate that candidate and present such candidate's name to the electorate who shall vote either for or against him in accordance with the provisions of this Act and the sole nominated candidate shall be declared winner if and only if he has attained more than fifty percent (50+1) of the total valid votes casted.*

2) Sheria ya Serikali za Mitaa (Uchaguzi) Sura 292 ya mwaka 1982 (Toleo la 2015)

Kuifuta kwa kuwa uchaguzi ukisimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi sheria hiyo inakosa uhalali wa kuwepo (redundant). Mamlaka ya uchaguzi yaliyomo katika sheria hiyo yahamishiwe Tume Huru ya Uchaguzi.

3) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka ya Wilaya) Sura 287 (Toleo la 2019

Kukifanyia marekebisho kifungu vya 37(1) vya sheria ili kisomeke ifuatavyo:

> *37.-(1) All elected members of the district council shall be elected at elections conducted for the purpose in accordance*

*with the provisions of the law **governing the Independent Electoral Commission** in relation to the election of members of local government authorities.*

4) **Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Sura 288**
Kukifanyia marekebisho kifungu cha 22 cha sheria ili kisomeke ifuatavyo:

*22.-1) All elected members of the district council shall be elected at elections conducted for the purpose in accordance with the provisions of the law **governing the Independent Electoral Commission** in relation to the election of members of local government authorities.*

5) **Sheria ya Jeshi la Polisi (Police Force and Auxilliary service Act Cap 322 of 1973)**
Kuifanyiwa marekebisho makubwa ili kulitoa katika siasa na kujiegemeza kwenye CCM hasa kwa kuzingatia kuwa upatikanaji wake ulikuwa umefungamanishwa na chama hicho kimoja kilichokuwepo (1973).
Pia viangalie vyombo vingine vya ulinzi na usalama (JWTZ, Usalama wa Taifa, Jeshi la Kujenga Taifa na Idara Maalumu za SMZ) ili vfanye kazi zake kwa weledi bila kufungamanishwa na utashi wa kisiasa.

6) Marekebisho katika Mahakama za Jamhuri ya Muungano

Huwezi kuzungumzia mambo yanayohusiana na uchaguzi bila ya kuzungumzia Mahakama. Mahakama ndizo zilizopewa jukumu la kusikiliza na kufanya uamuzi

kuhusiana na malalamiko au pingamizi za uchaguzi katika hatua mbalimbali. Kwa msingi huo, marekebisho yanayohusu mfumo wa uchaguzi yanapaswa pia kuhusisha marekebisho ya Mahakama (Judicial Reforms).

ACT Wazalendo tunapendekeza kwamba utaratibu wa kuwapata majaji wa Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mahakimu ufanyiwe mapitio kwa kuhusisha na kuipa mamlaka zaidi Tume ya Utumishi wa Mahakama katika kufanya mapendekezo kwa Rais badala ya kushauriana naye tu. Kuwepo na utaratibu wa wazi wa nafasi kutangazwa na kuombwa, kufanyika kwa usaili wa wazi, na kuwepo na Kamati ya Uteuzi wa Majaji.

Mapendekezo yetu ni kuifanyia marekebisho Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Ibara ya 109 kuhusu uteuzi wa Jaji Kiongozi na majaji wa Mahakama Kuu na Ibara ya 118 kuhusu uteuzi wa Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Rufaa kama ifuatavyo:

Uteuzi wa Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Rufaa,

> *(1) Jaji Mkuu atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa majaji wa Mahakama ya Rufaa* ***waliopendekezwa kwake*** *na Tume ya Utumishi ya Mahakama baada ya kupitia taratibu za Kamati ya Uteuzi.*
>
> *(2) Majaji wa Mahakama ya Rufaa watateuliwa na Rais kutoka* ***miongoni mwa majina yaliyopendekezwa na*** *Tume ya Utumishi ya Mahakama baada ya kupitia taratibu za Kamati ya Uteuzi.*
>
> *(3) Muundo na utaratibu wa kazi wa Kamati ya Uteuzi wa Majaji utakuwa kama ulivyoainishwa kwenye Sheria iliyotungwa na Bunge.*

Uteuzi wa Jaji Kiongozi na Majaji wa Mahakama Kuu,

> *(1) Jaji Kiongozi atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Majaji wa Mahakama Kuu* ***waliopendekezwa kwake*** *na Tume ya Utumishi ya Mahakama baada ya kupitia taratibu za Kamati ya Uteuzi.*
>
> *(2) Majaji wa Mahakama Kuu watateuliwa na Rais kutoka* ***miongoni mwa majina yaliyopendekezwa na*** *Tume ya Utumishi ya Mahakama baada ya kupitia taratibu za Kamati ya Uteuzi.*
>
> *(3) Muundo na utaratibu wa kazi wa Kamati ya Uteuzi wa Majaji utakuwa kama ulivyoainishwa kwenye Sheria iliyotungwa na Bunge.*

(b) Uchaguzi wa Zanzibar

Pamoja na kwamba yamekuwapo maeneo yanayolalamikiwa, lakini kwa jumla Zanzibar ilikuwa tayari imepiga hatua katika maeneo mengi yanayohusiana na uchaguzi mpaka kufikia mwaka 2010. Hii ilitokana na utekelezaji wa makubaliano yaliyokuwa yamefikiwa katika muafaka wa kisiasa na maridhiano. Hata hivyo, kati ya 2015 na 2020 yalifanywa mabadiliko ya Katiba na sheria mbalimbali ambayo yalirudisha nyuma hatua zilizokuwa zimepigwa hapo awali. Kwa sasa, hali imekuwa mbaya zaidi kuliko hata ilivyo kwa upande wa Tanzania Bara. Maoni ya ACT Wazalendo kuhusiana na uchaguzi wa Zanzibar ni kama ifuatavyo:

Katiba ya Zanzibar na sheria ya kuanzisha Tume ya Uchaguzi Zanzibar:

1. Kufanya marekebisho ya ibara ya 119(1) ya Katiba ya Zanzibar inayohusu muundo wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) ili kuifanya kuwa **Tume Huru ya**

Uchaguzi ambapo Mwenyekiti na Makamishna wawe wanapatikana kwa kuomba nafasi hizo na kisha kufanyiwa usaili na **Kamati ya Uteuzi** katika mtindo wa uwazi na unaozingatia maadili ya majukumu makubwa wanayokabidhiwa na Taifa. Sifa na vigezo viwekwe kwa Mwenyekiti na Makamishna wa Tume ambapo watatakiwa kuthibitisha bila kuacha chembe ya shaka kwamba ni watu waadilifu na wasio na rekodi ya kuwa na upande wowote wa siasa za vyama. Kamati ya Uteuzi itapitia majina ya walioomba, kuwasaili na kisha kupendekeza kwa Rais wa Zanzibar kwa uteuzi. Ibara ndogo ya 2 iwe ya 3 na iandikwe ibara ndogo ya 2 inayoainisha muundo wa Kamati ya Uteuzi wa wajumbe wa Tume ambayo itakuwa na wajumbe saba (7) kama inavyofafanuliwa hapa chini.

Mfumo huu unachanganya mifumo inayotumika kupata Tume Huru za Uchaguzi nchini Kenya na Afrika Kusini (kuhusiana na nafasi kutangazwa na kuombwa na kisha kufanyiwa usaili na Kamati ya Uteuzi) na pia ule unaotumika Uingereza katika kuwapata Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi wale tu waliokubaliwa na vyama vyote vyenye uwakilishi kwenye Bunge la Uingereza (House of Commons) ndiyo hatimaye hupitishwa na kuteuliwa kuwa Wajumbe wa Tume ya Uchaguzi.

Kwa hiyo ibara ya 119 inapendekezwa baada ya marekebisho isomeke ifuatavyo:-

> *119.(1) Kutakuwa na **Tume Huru ya Uchaguzi** ya Zanzibar **ambayo itasimamia uchaguzi wa Rais, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na Madiwani** ambayo itakuwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wengine watano (5) watakaoteuliwa na Rais kutokana na mapendekezo ya **Kamati Maalumu ya Uteuzi*** (selection panel) *ambayo muundo wake utakuwa kama unavyofafanuliwa kwenye kifungu cha (2) cha Ibara hii.*

(2) Iongezwe ibara ndogo 119(2) inayobainisha watakavyopatikana wajumbe wa Kamati ya Uteuzi itakayotangaza nafasi, kupokea maombi ya wanaoomba kuwa Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi, kuwafanyia usaili na kuwasilisha majina yaliyopendekezwa kuteuliwa na Rais kuwa wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi kama ifuatavyo:-

Kamati ya Uteuzi itakuwa na wajumbe (7) wafuatao:

a) Wajumbe wawili kutoka Majaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar watakaopendekezwa na Tume ya Utumishi ya Mahkama kwa kuzingatia jinsia na kukubaliwa na Vyama vya Siasa vyenye Uwakilishi kwenye Baraza la Wawakilishi,,

b) Wajumbe wawili kutoka Asasi za Kitaifa za masuala ya Sheria na Haki za Binaadamu watakaopendekewa na asasi hizo na kukubaliwa na Vyama vya Siasa vyenye Uwakilishi kwenye Baraza la Wawakilishi,

c) Wajumbe wawili kutoka Chama cha Wanasheria wa Zanzibar (Zanzibar Law Society) watakaopendekezwa na chama hicho (kwa kuzingatia jinsia) na kukubaliwa na Vyama vya Siasa vyenye Uwakilishi kwenye Baraza la Wawakilishi,

d) Mjumbe mmoja kutoka Chama cha Wanasheria Wanawake Zanzibar atakayependekezwa na chama hicho na kukubaliwa na Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi kwenye Baraza la Wawakilishi.

Madaraka ya kudhibiti nidhamu ya watu hao na madaraka ya kuwaondoa kazini yatakuwa mikononi mwa Kamati Maalumu ya Uteuzi iliyotajwa katika ibara ndogo ya (1) ya

ibara hii kwa utaratibu ule ule wa kuwandoa majaji wa Mahakama Kuu madarakani.

2. Ibara ndogo ya 119(13) ifutwe kwani inakinzana na ibara ya 12 ya usawa mbele ya sheria na kwamba shughuli za uchaguzi sio hatua inayochukuliwa na Serikali kwa lengo la kurekebisha matatizo mahsusi katika jamii.

3. Mkurugenzi wa Uchaguzi ambaye ndiye Katibu wa Tume Huru ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) apatikane kwa maombi ya kazi hiyo na kupendekezwa kwa Rais na Tume ya Uteuzi kwa ajili ya uteuzi.

4. Maofisa wengine wa ZEC ikiwa ni pamoja na wasimamizi na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi (Returning and Assistant Returning Officers), maofisa wa uchaguzi (Polling Officers) na makarani wa uchaguzi (Polling Clerks) wateuliwe kwa utaratibu wa maombi ya wazi na kufanyiwa usaili na makamishna wa ZEC wakishirikiana na Tume ya Uteuzi baada ya sifa na vigezo vyao kuainishwa pia kwa njia za wazi.

5. Uwekwe utaratibu wa kumuondoa Mwenyekiti au Kamishna wa ZEC, Mkurugenzi wa Uchaguzi au afisa yeyote wa ZEC atakayepoteza sifa na vigezo vya uadilifu vilivyowekwa na kisha nafasi yake kujazwa kwa utaratibu uleule tulioupendekeza hapo juu. Inapendekezwa utumike utaratibu uleule unaotumika kumuondoa jaji wa Mahakama Kuu.

6. Ibara ndogo za 120(1 & 4) za Katiba ziweke wazi kuhusu ukataji wa majimbo na wadi za uchaguzi na mipaka yake kwamba kazi hiyo itafanyika sio chini ya miaka 10 na kwa kufuata kikamilifu masharti yaliyowekwa na Katiba badala ya ukataji holela unaofanyika sasa kwa kuzingatia maslahi ya kisiasa ya chama kimoja. Mamlaka ya kugawa wadi na mipaka yake (ambako madiwani ndio huchaguliwa) yaondolewe kwa waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa (ambaye ni mwanasiasa na moja kwa moja ana maslahi ya kisiasa

katika ukataji wa wadi na mipaka hiyo) na mamlaka hayo yawekwe kwa mamlaka ya Tume Huru ya Uchaguzi.

Ibara hiyo isomeke:

> *120.(1) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, Zanzibar inaweza kugawanywa katika majimbo* ***na wadi*** *za uchaguzi zenye majina na mipaka kama yatakavyoelezwa na Tume Huru ya Uchaguzi.*
>
> *(4) Katika kipindi kisichopungua miaka 10 Tume itachunguza idadi ya mipaka na majina ya majimbo* ***na wadi*** *kwa kiwango kile ambacho inahisi ni wajibu kuangaliwa upya, na inaweza kwa kutoa tangazo, kubadili idadi, mipaka na majina ya majimbo na wadi hizo.*

7. Kwa hatua ya sasa, ukataji wa majimbo na wadi umefanywa kisiasa mno. Tunapendekeza majimbo ya uchaguzi na wadi kwanza yarudi kama yalivyokuwa mwaka 2010 kabla ya hatua zaidi za marekebisho ya msingi kufanywa.

8. Ibara ya 67 ya Katiba ya Zanzibar inayohusiana na upatikanaji wa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanaotokana na viti maalumu vya wanawake ifutwe ili kuondosha utatanishi uliopo katika kufanya hesabu ya uwiano ambapo kwa sasa kuna nafasi mbili ziko wazi na zinashindwa kujazwa na ZEC kwa sababu kila chama kati ya vyama vyenye uwakilishi Barazani kinajikuta hakijatimiza hesabu inayotakiwa. ACT Wazalendo tunapendekeza ubadilishwe mfumo wa uchaguzi kutoka wa sasa wa kumchagua mgombea wa chama (***majoritarian/post past the post)*** kwenda wa uwakilishi ***(proportional representation).*** Mfumo huo mpya unawezesha kupata 50/50 baina ya wanaumme na wanawake katika Baraza la Wawakilishi.

9. Ibaya ya 66 ya Katiba ya Zanzibar inayohusu uteuzi wa wajumbe 10 wa Baraza la Wawakilishi wanaoteuliwa na Rais wa Zanzibar ifanyiwe marekebisho kwa kuzingatia

kuwa uteuzi huo ufanywe kwa mujibu wa uwiano wa viti ambavyo vyama vya siasa vitapata kupitia uchaguzi mkuu. Hii itakuwa inakwenda sambamba na dhamira ya kuwepo kwa muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar. Mapendekezo yetu ni kwamba ibara hiyo isomeke ifuatavyo:

> *66. Kutakuwa na wajumbe kumi wa kuteuliwa wa Baraza la Wawakilishi ambao watateuliwa na Rais* ***kwa kushauriana na Makamu wote wa wawili wa Rais au Kiongozi wa Upinzani au vyama vyenye uwakilishi Barazani****, kwa kuzingatia* ***uwiano wa viti vya majimbo kwa vyama vya siasa vilivyomo ndani ya Baraza la Wawakilishi,*** *kutoka miongoni mwa watu wenye sifa zilizoelezwa na kifungu cha 68(a) na (c) cha Katiba ambao wakiteuliwa watafaa kuwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.*

1) **Kuhusu Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar:** Tunapendekeza kifungu cha 82 katika Sheria ya Uchaguzi kifutwe kuondoa utaratibu wa Kura ya Mapema ambao ulianzishwa katika uchaguzi mkuu wa 2020 na ukawa ndiyo chanzo na sababu ya vurugu na mchafuko yaliyopelekea watu 21 kuuawa Zanzibar (17 Pemba na 4 Unguja). Utaratibu huo haukuwa na sababu yoyote ya msingi ya kuanzishwa zaidi ya kutaka kuhujumu Uchaguzi. Tokea Uchaguzi Mkuu wa mwanzo wa vyama vingi mwaka 1995, Zanzibar imekuwa ikifanya uchaguzi siku moja tu na hakujawahi kuwa na malalamiko yoyote kuhusiana na utaratibu huo. Isitoshe, inashangaza kwamba Zanzibar yenye wapiga kura wasiozidi 500,000 iwe na siku mbili za kupiga kura wakati Tanzania Bara yenye wapiga kura 29,754,699 iwe inapiga kura siku moja tu. Kura ya Mapema ni chanzo cha majanga na machafuko na inapaswa kuondolewa kwenye Sheria ya Uchaguzi.

Kifungu hicho cha 82 cha Sheria ya Uchaguzi Zanzibar kinasomeka ifuatavyo:

> *82(1) Tume itaweka utaratibu utakaoruhusu upigaji kura wa mapema ambao utafanyika siku moja kabla ya siku ya upigaji kura, au siku nyengine yoyote kama itakavyoamuliwa na Tume*

Utaratibu wa kura ya mapema unaleta mkanganyiko/maswali wa/ya aina mbili;

a) Ikizingatiwa kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano (NEC) inatumia Daftari la kudumu la Wapiga Kura linalotumiwa na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar katika uendeshaji wa uchaguzi upande wa Zanzibar kwa mujibu wa Kifungu cha 12A (1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi Sura ya 343 Ni utaratibu gani Tume (NEC na ZEC) zinatumia kudhibiti wapiga kura waliokwishapiga Kura ya mapema wasirudie kupiga kura siku ya kupiga kura.

   Kifungu cha 12A(1) cha sheria ya uchaguzi Sura 343 kinabainisha:-

   > *12A(1) Notwithstanding the provisions of section 12, for the purposes of the conduct of the Parliamentary and Presidential elections in Tanzania Zanzibar, the law relating to the registration of voters and the register of voters for elections to the House of Representatives of Zanzibar shall mutatis mutandis be the law for the registration of voters and the register of voters in Tanzania Zanzibar for the purposes of this Act.*

b) Kifungu cha 82(1) kinaruhusu kura ya mapema kupigwa siki nyingine yoyote. Ikiwa kura ya mapema itatangazwa kufanyika mwezi mmoja au juma moja kabla ya siku ya kupiga kura dhamana ya kura zilizopigwa inakuwa mikonini mwa nani? Huu sio mwanya wa kuzichezea kura?

2) Ibara ya 128 ya Katiba kufanyiwa marekebisho kuipa mamlaka Tume Huru ya Uchaguzi kusimamia uchaguzi wa serikali za Mitaa. Inapendekezwa ibara hiyo isomeke ifuatavyo:-

> *128. Kutakuwa na Serikali za Mitaa ambazo uchaguzi wa viongozi wake* ***utasimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi****, madaraka na kazi za kila Serikali ya Mtaa zitakuwa kama zitavyoelezwa na Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.*

3) Kifungu cha 110(1) cha sheria ya uchaguzi kinachozuia matokeo ya uchaguzi wa Rais wa Zanzibar kupingwa Mahakamani kifanyiwe marekebisho ili matokeo hayo yaweze kuhojiwa na kupingwa Mahakamani kama ilivyo kwa matokeo mengine ya uchaguzi. Maoni yetu ni kuwa kifungu cha 110 cha sheria ya uchaguzi Zanzibar kifanyiwe marekebisho na kisomeke ifuatavyo:-

> *110(1) Malalamiko yanayohoji uhalali wa uchaguzi wa* ***Rais,*** *Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Diwani yataamuliwa na Mahakama Kuu.*

4) Vifungu vya 14(1) na (2) vya Sheria ya Uchaguzi vinavyomfanya Sheha kuwa wakala wa Tume na hivyo kumpa uwezo kuamua nani aandikishwe na nani asiandikishwe kuwa mpiga kura vifutwe. Masheha wasihusishwe kabisa na masuala ya uchaguzi kwa sababu wote ni watu walioteuliwa kwa kuzingatia ukereketwa wa Chama kinachotawala na wamekuwa chanzo na sababu ya hujuma kwenye uchaguzi. Sheria za Zanzibar tayari zimeweka sharti la mtu kuwa na Kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi (ZAN ID) ili kuandikishwa kuwa mpiga kura. Kwa utaratibu uliowekwa na Sheria za Zanzibar, mtu hasajiliwi wala kupatiwa kitambulisho cha Mzanzibari Mkaazi (ZAN ID) kama hajathibitishwa na Sheha. Kwa hivyo, kuweka utaratibu wa Sheha kuwemo kwenye vituo vya uandikishaji wa wapiga kura na kumpa jukumu la kuamua nani wa kupewa haki hiyo na nani wa kunyimwa ni usumbufu tu wakati tayari mtu amekuja na ZAN ID ambayo asingeipata kama hakuthibitishwa na Sheha. Mawakala wa vyama vya siasa wanaokuwemo kwenye vituo vya kuandikisha wapiga kura wanatosha kufanya kazi ya kuwatambua wapiga kura na kuwapinga wasio na sifa.

Kifungu cha 14 cha Sheria ya Uchaguzi Zanzibar kinasema:-

> *14(1) Sheha kutokana na wadhifa wake atakuwa ni wakala wa Uandikishaji wa Tume katika shehia yake.*
>
> *(2) Kila Sheha au mwakilishi wake katika Shehia ambayo kituo cha uandikishwaji*

kimeanzisha, atashirikiana na Afisa Uandikishaji au Karani wa Uandikishaji kuhakikisha uasimamizi mzuri wa sheria na kanuni zinazohusiana na Uandikishaji wa wapiga kura katika kituo.

Aidha utaratibu wa sheha kuamua nani aandikishwe na nani asiandikishwe kwa kuzingatia itikadi za kisiasa ni uvunjaji wa masharti ya Katiba ya Zanzibar katika ibara 25(1) yanayobainisha haki za lazima na uhuru binafsi kama ifuatayo:-

25.(1) Ilivyokuwa kila mtu wa Zanzibar anawajibika kupata haki zake za lazima na uhuru wa binafsi bila ya kujali kabila, pahali alipotoka au maskani au mahusiano mengine yoyote yale, mtazamo wa kisiasa alionao, rangi, dini au jinsi, lakini mradi iwe uhuru wake unaheshimu haki na uhuru wa wengine na iwe kwa faida ya jamii,

5) Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar inapaswa kuweka wazi kwamba majumuisho ya kura yatafanyika ndani ya jimbo husika kama ilivyokuwa kabla badala ya utaratibu uliowekwa sasa wa kufanya majumuisho kwenye Ofisi za Wilaya. Utaratibu huo chini ya kifungu 93(1) cha Sheria ya Uchaguzi; ambao hupelekea kulazimika kusafirisha masanduku ya kura kwenda Ofisi hizo za Wilaya, umekuwa chanzo kikubwa cha vurugu na hata watu kupoteza maisha katika Uchaguzi Mkuu wa 2020.

Inapendekezwa kifungu hicho kirekebishwe na kusomeka ifuatavyo:-

> *93(1) Msimamizi wa Uchaguzi kwa kufuata miongozo ya Tume, atachagua eneo katika* ***jimbo kuwa kituo cha majumuisho ya kura na atafanya majumuisho na kutangaza matokeo.***

6) Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar inapaswa kuweka wazi kwamba watakaokuwa na dhamana ya kulinda vituo vya uchaguzi na maeneo yote yanayohusika na uchaguzi watakuwa ni Polisi ambao ndiyo wenye jukumu la kulinda usalama wa raia na mali zao na waliopewa mafunzo ya kazi hiyo. Utaratibu wa kutumia askari wa jeshi la JWTZ pamoja na Idara Maalum za SMZ (Vikosi vya SMZ) haukubaliki na unapaswa kuondoshwa hasa kwa kuzingatia kuhusika kwao katika vurugu za uchaguzi Zanzibar. Inapendekezwa kuvifanyia marekebisho vifungu vya 77(1)(e) na 77(2)(d) vya Sheria ya Uchaguzi ili visomeke ifuatavyo:-

> *77(1)(e) Afisa wa Polisi kwa madhumuni ya kusimamia usalama katika zoezi la kupiga kura.*
>
> *(2)(d) Afisa wa Polisi kwa madhumuni ya kusimamia usalama katika zoezi la kuhesabu kura.*

7) Sheria iweke utaratibu wa wazi wa kushughulikia rufaa dhidi ya maamuzi yanayofanywa na ZEC. Tunapendekeza kuwepo na chombo huru cha kusikiliza ***rufaa (Adjudication Panel)*** dhidi ya maamuzi yanayofanywa na ZEC ili kupunguza

malalamiko dhidi ya maamuzi yasiyozingatia sheria yanayofanywa na ZEC kama ilivyokuwa kwenye uchaguzi mkuu wa 2020. Maoni yetu ni kuundwa kwa chombo hicho, kurekebisha kifungu vya 17(5), kuongeza kifungu cha137(4) na kufuta kifungu143 cha Sheria ya Uchaguzi. Vifungu 17(5) na 137(4) visomeke ifuatavyo:-

> *17(5) Iwapo muombaji hakuridhika na uamuzi wa Tume, atakata Rufaa kwa **Adjudication Panel** ambayo itasikiliza na kutoa uamuzi ndani ya siku kumi na nne na uamuzi wake unaweza kukatiwa Rufaa Mahakama yenye uwezo **(jurisdiction)** kwa kadri itakavyokuwa.*
>
> *137(4) Endapo Mgombea au Mwakilishi wake aliyewasilisha malalamiko hakuridhika na uamuzi wa Tume, atakata Rufaa kwa **Adjudication Panel** ambayo itasikiliza na kutoa uamuzi ndani ya siku kumi na nne na uamuzi wake unaweza kukatiwa Rufaa Mahakama yenye uwezo **(jurisdiction)** kwa kadri itakavyokuwa.*

8) Sheria iweke wazi kuhusu utaratibu wa kuwapata wanaotoa huduma za kutengeneza vifaa vya uchaguzi ***(election materials)*** ikiwa ni pamoja na uchapishaji wa karatasi za uchaguzi ***(ballot papers),*** wino usiofutika, mihuri ya ZEC inayotumika kwenye uchaguzi, na vifaa vyengine vyote vinavyohusika na uchaguzi. Utaratibu huo uwe wazi na usiwache mashaka yoyote juu ya uwezekano wa kufanyika hujuma au ufisadi katika upatikanaji wa vifaa hivyo.

9) Sheria ya Uchaguzi iweke wazi kabisa katika lugha isiyo na utatanishi kuhusu haki za mawakala wa vyama vya siasa na mawakala wa wagombea katika mfumo wa uchaguzi. Hili lifanyike ili kuondoa hali inayofanyika sasa ya maofisa wa ZEC au Polisi au hata maofisa wengine wa vyombo vya ulinzi na usalama kuwatoa nje ya vituo mawakala wa vyama au wagombea wa upinzani pale wanapotetea maslahi ya vyama vyao/wagombea wao ambalo ndilo jukumu lao la msingi. Ni maoni yetu kuwa yafanyike marekebiso katika kifungu cha 75 kwa kuongeza fasili mbili (6 & 7) na kurekebisha kifungu cha 76 ili kumlinda wakala kuodolewa kituoni. Mapendekezo ya marekebisho hayo ni kama ifuatavyo:-

> *75(6) Wakala aliyeteuliwa na chama cha siasa kuwemo katika kituo cha Uandikishaji, upigaji, uhesabuji au ujumulishaji kura, hataondolewa na mtu au chombo chochote, isipokuwa Msimamizi wa Uchaguzi baada ya kushauriana na chama husika.*
>
> *75(7) Wakala aliyeondolewa chini ya fasili (6) ya kifungu hichi, anaweza kubadilishwa na mwingine aliyekula kiapo kwa mujibu wa masharti ya sheria hii.*
>
> *76. Endapo katika Sheria hii jambo au kitu kinachohitajika au kimeamuriwa kushuhudiwa na wakala hakikushuhudiwa kwa wakala kushindwa kuwepo au kutohudhuria katika muda, mahali na wakati*

ulioteuliwa kwa jambo hilo, kutokuwepo kwa wakala hakutabatilisha uamuzi wa Msimamizi wa Uchaguzi ***isipokuwa wakala ameondolewa bila kuzingatia masharti ya kifungu 75 (6).***

10) Sheria ya Uchaguzi iweke wazi kwamba zoezi la upigaji kura katika vituo vya kupigia kura halitaanza bila ya vifaa vyote vya uchaguzi (zikiwemo fomu zote za uchaguzi) vinavyotakiwa kuwepo viwe vipo kwenye kituo husika. Inapendekezwa kuifanyia marekebisho fasili 69(b) ili isomeke ifuatavyo:-

> *69(b) Kuna vifaa na nyaraka za kutosha za* ***kupigia kura, kuhesabu kura, matokeo na malalamiko ya uchaguzi na hataruhusu kuanza kupiga kura bila vifaa hivyo vya uchaguzi kukamilika.***

11) Sheria ya Uchaguzi iweke wazi kwamba Wasimamizi wa Uchaguzi na Wasimamizi Wasaidizi wa Uchaguzi watawaapisha Mawakala wote wa Uchaguzi na kuwapatia Shahada/Vyeti vya Utambulisho angalau siku tatu kabla ya siku ya uchaguzi. Tunapendekeza kuwepo kwa fasili mpya (j) chini ya kifungu inayobainisha majukumu ya Wasimamizi wa Uchaguzi na fasili hiyo isomeke ifuatavyo:-

> *68(j) Kwa kushirikiana na Wasimamizi wa vituo kuwaapisha kiapo cha kutunza siri na kuwapa vyeti vya utambulisho mawakala walioteuliwa na vyama vinavyoshiriki uchaguzi siku tatu kabla ya siku ya uchaguzi.*

Fasili 68(j) ya awali ibadilishwe kuwa 68(k).

12) Sheria ya Uchaguzi iweke wazi haki ya wagombea kuwemo katika vituo vya uchaguzi, vituo vya kuhesabia kura na vituo vya majumuisho ya kura na kushuhudia hatua zote za uchaguzi, jambo ambalo kwa sasa halizingatiwi na lilihujumiwa kwa kiasi kikubwa katika Uchaguzi Mkuu wa 2020. Aidha uwepo wa fasili 77(1)(i) kumekuwa ni sababu ya vituo vya uchaguzi, uhesabuji na ujumlishaji kura kuvamia na watu wasihusika na uchaguzi kwa visingizio mbali mbali ikiwemo vya kuwa Kamati za Ulinzi na Usalama na kuingilia mchakato wa uchaguzi. Maoni yetu ni kuondoa fasili(i) na kuboresha kifungu kidogo cha 77(3) ili kisomeke ifuatavyo:-

> *77(3) Hakuna mtu mwingine yeyote ukiachilia waliotajwa katika vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki, atakayeruhusiwa kuwa ndani ya eneo la mita mia mbili la kituo cha kupigia, kuhesbu au* ***kujumlisha*** *kura.*

Kifungu kidogo cha 123(x) kifanyiwe marekebisho kufanya kuwa miongoni mwa makosa kuondolewa wakala/mgombea katika kituo na kisomeke ifuatavyo:-

> *123(x) Akiwa Msimamizi au Msimamizi wa kituo cha kupigia kura akijua au kwa uzembe akashindwa kuweka alama inayokubaliwa katika karatasi ya kura, kumwondoa wakala au mgombea kituoni bila kuzingatia matakwa ya Sheria ya Uchaguzi;*

13) Sheria ya Uchaguzi ifanyiwe marekebisho ili kuondoa uenguaji holela wa wagombea wa upinzani kupitia pingamizi zisizo na msingi, jambo ambalo lilifurutu ada katika Uchaguzi Mkuu wa 2020. Sababu na hoja za pingamizi dhidi ya wagombea zinapaswa kutizamwa upya ili kuondoa sintofahamu zinazojitokeza (***absurdity)***.

Kwa maoni yetu chanzo cha tatizo hilo ni matakwa ya fasili (a) ya kifungu kidogo 51(1) ambayo tunapendekeza ifutwe. Fasili hiyo inatamka ifuatavyo:-

> *51(1(a) Taarifa za mgombea zilizotajwa hazitoshelezi kumtambua mgombea.*

Vifungu vya 43, 44 na 45 vya Sheria ya Uchaguzi vimeainisha sifa za mgombea Urais, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na Diwani. Katiba ya Zanzibar katika ibara ya 69 imebainisha sababu za kutofaa kuwa mgombea. Hayumkiniki pingamizi kuwa nje ya matakwa ya sheria na Katiba. Fasili 51(1)(a) ndiyo inawapa Wasimamizi wa Uchaguzi/Wasimamizi wa vituo kukubali mapingamizi ya hovyo hovyo na hivyo kuwaengua wagombea wa vyama vya upinzani.

14) Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar inapaswa kulifanya kuwa ni kosa la jinai utaratibu wa wagombea au watu wengine wanaotoa au kuweka pingamizi kwa kutumia nyaraka za siri ambazo zinapaswa kuwa katika mamlaka za kiserikali na ambazo wahusika huwa wamezitoa kwa kuzingatia haki yao ya faragha.

Lilikuwa ni jambo la kawaida ambalo linatia aibu katika Uchaguzi Mkuu wa 2020 kwamba mamlaka za Serikali kama vile NIDA, Uhamiaji, Mamlaka za Uajiri Serikalini, Ofisi za Usajili wa Vyeti vya Kuzaliwa, Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar na nyinginezo kama hizo kutoa nyaraka na kuwapa wagombea wa CCM ili kuzitumia kuwekea pingamizi dhidi ya wapinzani. Jambo hili ni uhalifu mkubwa na linapaswa kuwekwa wazi katika Sheria ya Uchaguzi kwamba litakuwa ni kosa la jinai. Tunapendekeza kifungu cha 119(1) kiongezwe fasili(g) ambayo itatamka ifuatavyo:-

> *119(1)(g) atatoa nyaraka za siri za serikali, idara au mamlaka yoyote ambazo hutolewa kwa kuzingatia haki ya faragha ya mtu, kwa jili ya kumwekea pingamizi mgombea yeyote.*

15) Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar iweke wazi kwamba Mwenyekiti wa ZEC au Ofisa yeyote wa Tume hana mamlaka ya kufuta uchaguzi bila ya ridhaa ya Tume ya Uchaguzi kupitia kikao halali na kwa kufuata vigezo na masharti yatakayowekwa na pia kwamba hatua kama hiyo haiwezi kufanyika baada ya kura kuhesabiwa na fomu za matokeo kujazwa au baada ya matokeo kutangazwa. Tunapendekeza kuvifanyia marekebisho vifungu 93(6)(a) na 96(3) vya Sheria ya Uchaguzi kusomeka ifuatavyo:-

> *93(6)(a) Atatangaza kura zote zilizopigwa kwa kila mgombea na atamtangaza mara moja, mgombea*

aliyepata kura nyingi kuwa amechaguliwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Diwani kwa kadri itakavyokuwa na ushindi huo hautabatilishwa na mtu yeyota isipokuwa kwa uamuzi wa Mahakama.

96(3) Tume itamtangaza mshindi wa uchaguzi wa Urais aliyepata kura nyingi halali zilizopigwa, ushindi ambao hautabatilishwa na mtu yeyote isipokuwa kwa uamuzi wa Mahakama.

16) Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar irekebishwe kwa kufuta kifungu kinachokataza mawakala wa vyama kuingia na vifaa vya kielektroniki ndani ya vituo vya kupigia kura, kuhesabu na kufanya majumuisho ya kura ambacho kimsingi lengo lake lilikuwa ni kuwazuia mawakala kuweza kuwasiliana na wagombea na vyama vyao wanavyoviwakilisha, jambo ambalo haliashirii dhamira njema ya kuhakikisha uchaguzi unakuwa huru, wa haki na ulio wazi (free, fair, credible and transparent elections). Uchaguzi unaofanywa gizani ndiyo chanzo cha kutiliana shaka na kuzaa hujuma na vurugu.

17) Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar iweke wazi kwamba kila Chama cha Siasa kinachoshiriki Uchaguzi kitapatiwa nakala ya Daftari la Wapiga Kura kwa mfumo wa kielektroniki likiwa na taarifa zote za wapiga kura pamoja na picha zao angalau siku 30 kabla ya siku ya kupiga kura.

Tunapendekeza kuongezwa kifungu kidogo cha 28(10) kitakacho itaka Tume ya Uchaguzi

kusambaza nakala ya kieleroniki ya DKWK vyama vya vyote vya siasa na ofisi ya Msajili wa vyama vya siasa kwa maneno yafuatayo:-

> *28(10) Tume itahakikisha kuwa nakala ya kielectroniki ya Daftari la Wapiga Kura (DKWK) inavifikia vyama vyote vya siasa na ofisi ya Msajili wa vyama vya siasa si chini ya siku 30 kabla ya tarehe iliyotangazwa kuwa siku ya uchaguzi*

18) Kifungu cha 112(2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar kinachohusu malipo ya gharama za uwasilishaji wa malalamiko ya uchaguzi (election petition) dhidi ya Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi (shilingi milioni mbili) na Diwani (shilingi laki tano) na pia vifungu vingine vinavyohusu gharama za kuweka pingamizi na mambo mengine yanayohusiana na uchaguzi (shilingi laki tatu) - vyote vifutwe ili kuondoa masharti hayo. Hoja yetu ni kwamba masuala ya uchaguzi ni haki ya msingi ya raia katika kuchagua na kuchaguliwa na kuwaweka madarakani viongozi watakaowaongoza na hivyo haitakiwi kuwekewa vikwazo vya malipo ya fedha katika kuitekeleza haki hiyo.

Kuhusiana na Sheria nyinginezo:

1. Sheria ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ifanyiwe marekebisho na kuondoa madaraka ya waziri mwenye dhamana ya Serikali kuamua idadi na mipaka ya wadi za uchaguzi kwa sababu wadi ndizo zinazotoa madiwani na hili ni zoezi lenye maslahi ya kisiasa sio sahihi kazi hii kuachiwa waziri ambaye ni mwanasiasa. Mamlaka ya kuamua idadi ya wadi inapaswa kuwa chini ya ***Tume***

Huru ya Uchaguzi ambayo ndiyo yenye dhamana ya idadi na mipaka ya majimbo ya uchaguzi.

2. Kufuta shehia na kubakiza wadi tu kama muundo wa chini kabisa wa Serikali za mitaa. Kwa sasa Zanzibar kuna wadi 111 zenye madiwani wanaochaguliwa na kuna shehia 397 zenye masheha wanaoteuliwa. Bahati mbaya masheha wanaoteuliwa wamepewa mamlaka makubwa na yote ambayo ungetegemea yafanywe na madiwani wanaochaguliwa na wananchi. Hili limesababisha pia ongezeko kubwa la gharama za kuhudumia muundo huo ambao hauhitajiki na hauna tija. Tunapendekeza kwamba katika kuimarisha demokrasia, ngazi ya chini iwe ni ya wadi ambayo viongozi wake (madiwani) wanachaguliwa na wananchi moja kwa moja.

Marekebisho katika Mahakama Zanzibar:

Huwezi kuzungumzia mambo yanayohusiana na uchaguzi bila kuzungumzia Mahakama ambazo zimepewa jukumu la kusikiliza na kufanya uamuzi kuhusiana na malalamiko au pingamizi za uchaguzi katika hatua mbalimbali. Kwa msingi huo, marekebisho yanayohusu mfumo wa uchaguzi yanapaswa pia kuhusisha marekebisho ya Mahakama (Judicial Reforms).

ACT Wazalendo tunapendekeza kwamba utaratibu wa kuwapata Majaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar na Mahakimu ufanyiwe mapitio kwa kuhusisha na kuipa mamlaka zaidi Tume ya Utumishi wa Mahakama katika kufanya mapendekezo kwa Rais badala ya kushauriana naye tu. Kuwepo na utaratibu wa wazi wa nafasi kutangazwa na kuombwa, kufanyika kwa usaili wa wazi, na kuwepo na Kamati ya Uteuzi wa Majaji. Mapendekezo yetu ni kuzifanyia marekebisho ibara za 94(1 & 2) za Katiba na kuongeza Ibara ndogo ya (3) ili zisomeke kama ifuatavyo:-

> *94.(1) Jaji Mkuu atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa Majaji wa Mahkama Kuu*

waliopendekezwa kwake *na Tume ya Utumishi ya Mahkama baada ya kupitia taratibu za Kamati ya Uteuzi.*

(2) Majaji wa Mahkama Kuu watateuliwa na Rais kutoka ***miongoni majina yaliyopendekezwa na*** *Tume ya Utumishi ya Mahkama baada ya kupitia taratibu za Kamati ya Uteuzi.*

(3) Muundo na utaratibu wa kazi wa Kamati ya Uteuzi wa Majaji utakuwa kama ulivyoainishwa kwenye Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi.

F. USHIRIKI WA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUMU KATIKA DEMOKRASIA YA VYAMA VINGI VYA SIASA

Ili kuwezesha ushiriki wenye tija wa wanawake na makundi maalumu katika demokrasia ya vyama vingi, sharti kubadilisha mfumo wa uchaguzi nchini. Mfumo wa sasa wa kumchagua mgombea wa chama ***(majoritarian/post past the post)*** hautoi fursa sawa za wanawake na makundi maalumu kushiriki kutokana na sababu za mila potofu, uwezo wa kiuchumi, kauli chafu wakati wa kampeni za uchaguzi na imani za kidini. Vilevile mfumo huo haujengi vyama imara vyenye kuweka wazi sera ambazo kwazo wapiga kura watavutika kuvipa ridhaa yao. Kimsingi vyama vinaingia katika uchaguzi bila kuwa na ilani zenye vipaumbele vinavyoeleweka kwa wapiga kura na hivyo kufifisha dhana ya ushindani wa sera. Hii ni miongoni mwa sababu za kampeni za kukashifiana, matusi na rushwa katika uchaguzi.

Kadhalika uchaguzi unakosa tafsiri ya utashi halisi wa wapiga kura kwani mshindi huchukua kila kitu ***(the winner takes it all)*** bila kuzingatia kuwa hata vyama vilivyoshindwa vilikuwa na asilimia fulani ya kukubalika kwa wapiga kura.

Kulielewa hili vizuri tuchukulie hali halisi ya uchaguzi wa Zanzibar ambapo vyama vinavyoshindana hupishana kwa kura chache (chama kilichoshinda kinapata 50.1% na chama pinzani kinashindwa kwa kupata 49.9% ya kura zote), kisha mshindi anachukua kila kitu. Hali hiyo haionyeshi uhalisia wa utashi wa wapiga kura katika serikali inayoundwa baada ya uchaguzi na hiyo inaweza kukwamisha shughuli za maendeleo na inaiweka rehani amani ya nchi. Kuna haja kubwa kuwa na maridhiano ya kitaifa ili kulinda misingi ya

waasisi wa nchi yetu ya **uhuru**, **haki, udugu na amani** ambayo imepewa nguvu katika dibaji za katiba zetu zote mbili.

Licha ya Katiba ya nchi katika ibara ya 66(1)(b) kuweka fursa kwa wanawake kushiriki siasa kupitia utaratibu wa viti maalumu, bado Tume ya Taifa ya Uchaguzi haijatekeleza masharti ya ibara ya 81 inayoitaka kuweka utaratibu wa namna gani uteuzi wa wanawake ufanywe kwa vyama vya siasa. Matokeo yake mpaka sasa kuna maswali ya ufanisi wa utaratibu wa utelezaji wa viti maalumu nchini miaka 36 baada ya kuanzishwa nchini.

Ibara ya 81 ya Katiba inasema:

> *81. Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya Katiba hii, Tume ya Uchaguzi yaweza kuweka masharti yanayofafanua utaratibu utakaotumiwa na vyama vya siasa kwa ajili ya kuchagua na kupendekeza majina ya wabunge wa aina iliyotajwa katika ibara ya 66(1) (b).*

Mfumo unaopendekezwa ni ule wa uwakilishi ***(proportional representation)*** ambapo kura huwa ni za chama badala ya mgombea. Mfumo huu unataka kila chama kuwasilisha kwa Tume Huru za Uchaguzi orodha ya wanachama wake kwa umuhimu ***(in order of preference)*** ambao wana sifa za kuwa wabunge/wawakilishi kwa sharti kuwa mmoja akiwa mwanaume, wa pili anakuwa mwanamke na lazima kuwa na asilimia fulani itakayokubalika kisheria ya makundi maalumu.

Chama wakati wa kampeni huuza sera zake ili kuwashawishi wapiga kura na kutokana na kukubalika kwa sera zake kupitia ilani, hupata kuungwa mkono na kupigiwa kura.

Kura zikihesabiwa huwekwa kwenye kapu la chama badala ya mgombea mmoja mmoja. Mwishowe hutafutwa uwiano wa kura miongoni mwa vyama vilivyoshiriki uchaguzi na viti vya Bunge/Baraza la Wawakilishi hugawanywa kwa kila chama kwa mujibu wa uwiano wa kura.

Chama chochote ili kuongoza serikali lazima kuwe na kiwango cha kura ambacho lazima kifikiwe. ACT Wazalendo tunapendekeza kiwango cha asilimia sitini (60%) ya kura zote halali zilizopigwa. Hii ni katika kuhakikisha kuwa kura za wananchi zinazingatiwa katika kuunda serikali.

Tunafahamu kuwa uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji na uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ni uchaguzi uliopindukia uchafuzi wa uchaguzi tangu kuanzishwa kwa uchaguzi wa vyama vingi mwaka 1995. Hata hivyo kama mfumo wa uwakilishi ungetumika idadi ya viti vya wabunge vingekuwa tofauti na ilivyo sasa. Mfano katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo lina majimbo 264 na kwa hiyo wabunge 264, kwa mgawanyo wa wabunge 214 Tanzania Bara na 50 Zanzibar na kama kila upande wa Jamhuri utajitegemea ili kuzingatia uwiano wa kura (kusudi Zanzibar isimezwe) mgawo wa viti kwa Tanzania Bara utakuwa kama ifuatavyo:

- Chama A kikipata 60% ya kura kitapata 60% ya viti (viti 128), chama B kilichopata 25% ya kura kitapata 25% ya viti (viti 54), chama C kilichopata 8% ya kura kitapata 8% ya viti (viti 17) na chama D kilichopata 7% ya kura kitapata 7% ya viti (15).

- Kwa upande wa Zanzibar viti vya ubunge; chama A kikipata 60% ya kura kitapata 60%

ya viti (viti 30), chama B kilichopata 25% ya kura kitapata 25% ya viti (viti 13), chama C kilichopata 8% ya kura kitapata 8% ya viti (viti 4) na chama D kilichopata 7% ya kura kitapata 7% ya viti (4).

- Zanzibar viti katika Baraza la Wawakilishi vitakuwa; chama A kikipata 60% ya kura kitapata 60% ya viti (viti 30), chama B kilichopata 25% ya kura kitapata 25% ya viti (viti 13), chama C kilichopata 8% ya kura kitapata 8% ya viti (viti 4) na chama D kilichopata 7% ya kura kitapata 7% ya viti (4).

Katika kuteua wabunge/wawakilishi wa chama, Tume Huru ya Uchaguzi itazingatia orodha iliyowasilishwa kwake na chama husika kwa mujibu wa kipaumbele (in order of preference). Orodha hiyo ya chama ndiyo itatumika kuteua wabunge/wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa chama endapo itatokea nafasi wazi kwa sababu zozote zile katika kipindi chote cha uhai wa Bunge na hivyo kuokoa gharama za kuitishwa uchaguzi mdogo.

Mfumo huo unaopendekezwa ndio unaweza kuleta suluhu ya haraka na yenye tija katika ushiriki wa wanawake na makundi maalumu katika siasa ya demokrasia ya vyama vingi. Pia mfumo huo ndio unawezesha utekelezwaji wa ibara ya tisa (9) ya Itifaki ya Maputo ambayo Tanzania iliiridhia mwaka 2007 (Article 9 of the Protocol to the African Charter on Human and Peoples' Rights on the Rights of Women in Africa (Maputo Protocol), inayosema:

> *(9) States Parties shall take specific positive action to promote participative governance and the equal participation of women in the*

political life of their countries through affirmative action, enabling national legislation
and other measures to ensure that:

a) women participate without any discrimination in all elections;

b) women are represented equally at all levels with men in all electoral processes; and

c) women are equal partners with men at all levels of development and implementation of state policies and development programmes.

Mfumo huo ndio unaotumika katika nchi ya Finland na umekuwa na tija sana.

Miongoni mwa faida za mfumo huo ni zifuatazo:

i. Unawezesha uwiano wa 50/50 kati ya wanaume na wanawake katika vyombo vya maamuzi kama Bunge, Baraza la Wawakilishi na mamlaka za Serikali za Mitaa na katika siasa za demokrasia ya vyama vingi.

ii. Unaodoa udhalilishwaji wa wanawake (rusha ya ngono) kupitia viti maalumu.

iii. Unawatambua wageni (wahamiaji wenye uraia) kama kundi maalumu na hivyo kuruhusiwa kushiriki siasa na kuchaguliwa kupitia vyama vyao ***(optional).***

iv. Unaondoa dhana ya mgombea kupita bila kupingwa.

v. Unaondoa utaratibu wa mfumo wa sasa unaoruhusu kuamua nani ashinde na nani asishindwe kwa vyama vya upinzani kupitia Tume ya Taifa ya Uchaguzi/ Wasimamizi wa Uchaguzi,

vi. Unarahisisha mchakato wa ushirikiano wa vyama wakati wa uchaguzi (***coalition)*** na uundwaji wa serikali za umoja wa kitaifa (vyama) pale ambapo hakuna chama kimoja pekee kilichopata kura za kukiwezesha kuunda serikali.

vii. Unapunguza gharama za uchaguzi wa marudio (uchaguzi mdogo) pale ambapo kwa sababu zozote kunatokea nafasi wazi.

viii. Unaondoa uwezekano wa kiti cha mbunge, mwakilishi, diwani au kiongozi wa serikali ya mtaa kuwa wazi kwa kipindi kirefu bila kujazwa.

ix. Unajenga vyama vya siasa imara na vyenye ustahimilivu ***(parties with capacity to stand up on the opinion of the other)*** na kuondosha utitiri wa vyama vibaraka ***(puppet parties).***

Jedwali lifuatalo linaonyesha mtiririko wa uwiano wa kura na idadi ya viti vya wabunge kwa vyama vilivyoshiriki uchaguzi mwaka 2020 kama ingezingatiwa mfumo wa uchaguzi wa uwakilishi;

TANZANIA BARA					**ZANZIBAR**			
CHAMA	**KURA**	**%**	**VITI**		**KURA**	**%**	**VITI**	**JUMLA KUU VITI**
CCM	8,591,202	75.7	162		309,487	70.5	35	**197**
CHADEMA	2,052,374	18.1	39		19,059	4.3	2	**41**

ACT	291,420	2.6	5		80,904	18.4	9	**15**
CUF	235,430	2.1	4		14,629	3.3	2	**6**
NCCR	67,498	0.6	1		1,050	0.2	0	**1**
CHAUMA	6,460	0.1	0		2,751	0.6	0	**0**
NRA	4,861	0.0	0		816	0.2	0	**0**
CCK	10,686	0.1	0		148	0.0	0	**0**
AAFP	8,926	0.1	0		854	0.2	0	**0**
UMD	2,237	0.0	0		221	0.1	0	**0**
DEMO-MAKINI	6,028	0.1	0		1,298	0.3	0	**0**
ADC	33,876	0.3	1		4,085	0.9	0	**1**
SAU	2,901	0.0	0		75	0.0	0	**0**
UDP	10,211	0.1	0		590	0.1	0	**0**
UPDP	3,491	0.0	0		747	0.2	0	**0**
ADA-TADEA	11,521	0.1	0		1,406	0.3	0	**0**
DP	3,126	0.0	0		238	0.1	0	**0**
NLD	511	0.0	0		126	0.0	0	**0**
TLP	3,111	0.0	0		293	0.1	0	**0**
Jumla	**11,345,870**	**100**	**214**		**438,777**	**100.0**	**50**	**264**

G. ELIMU YA URAIA

Licha ya kutajwa kuwa tatizo la msingi na ambalo linafanya hata uchaguzi kukosa tija kutokana na wananchi kutokuwa na elimu ya uraia na hivyo kushiriki uchaguzi bila kufahamu faida na madhara ya uongozi wanaoupigia kura, suala la elimu ya uraia limekosa kutiliwa nguvu na sheria zote mbili (NEC na ZEC) za uchaguzi. Sheria zetu za uchaguzi zinatambua elimu ya mpiga kura (voters' education which means dissemination of information relating to the electoral processes and procedures). Jambo hilo limefafanuliwa vizuri katika kifungu cha 4C cha Sheria ya Uchaguzi (NEC), vifungu vya 3 - 6 vya Kanuni za Uchaguzi chini ya sheria ya uchaguzi (NEC) na vifungu vya 106 – 108 vya sheria ya uchaguzi ya Zanzibar (ZEC).

Elimu ya uraia inatajwa pekee katika kifungu cha 4(5)(f & g) cha sheria ya vyama vya siasa (Toleo la 2019), ambapo ni jukumu la ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kutoa na kusimamia kutolewa kwa elimu ya uraia kwa vyama vya siasa. Vifungu hivyo vinasema:

> *4(5)(f) provide civic education regarding multiparty democracy, laws administered by the Registrar and related matters;*
>
> *(g)regulate civic education provided to political parties;*

Licha ya uhalisia kwamba ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa haina uwezo wa kutoa elimu hiyo na imekuwa kipingamizi cha kutolewa elimu na mafunzo mengi kwa vyama vya siasa, ni kwamba hata kama Msajili angekuwa na uwezo angeshughulika na sehemu ndogo sana ya wananchi wapiga kura kwani wanachama wa vyama vya siasa nchini ni takriban 10,000,000

(16.7%) tu ya Watanzania wote. Bila kuwa na mkakati mbadala elimu ya uraia kwa wananchi itachukua muda mrefu kuwafikia watanzania wote ili kuwawezesha kushiriki uchaguzi na ufahamu, hivyo kuepusha vitendo vya rushwa na uvunjifu wa maadili katika uchaguzi.

Maoni ya ACT Wazalendo katika suala hili ni kama ifuatavyo:-

i. Jukumu hilo badala ya kuwa la Ofisi ya Msajili, liwe la vyama vyenyewe na liainishwe katika katiba za vyama.

ii. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa isiingilie kwa kudhibiti mafunzo ya vyama vya siasa, bali ipewe taarifa ya kutolewa kwa mafunzo kama ambavyo inapendekezwa Jeshi la Polisi kupewa taarifa ya kufanyika mikutano ya hadhara.

iii. Iwe ni mada muhimu kwenye mikutano yote ya hadhara itakayofanywa na vyama vya siasa na awepo mtoa elimu maalumu aliyeandaliwa.

iv. Tume Huru za Taifa za Uchaguzi (NEC na ZEC) pamoja na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa waandae na kutoa mtalaa wa elimu ya uraia utakaotumiwa na vyama vya siasa kutoa elimu hiyo kwa wananchi.

Ili kuwezesha utekelezwaji wa jambo hilo tunapendekeza kukifanyia marekebisho kifungu cha (9), kwa kuongeza fasili ndogo 2(g) ili utoaji wa elimu ya uraia liwe sharti (condition for registration) la kuzingatiwa katika usajili wa chama cha siasa na miongoni mwa mambo muhimu kwenye katiba yake.

Tunapendekeza kiongezwe kipengele (s) kwenye jedwali la kwanza (First Schedule) vyote kwa pamoja visomeke ifuatavyo:

> *9(2)(g) It does not allow provision of civic education regarding multiparty democracy, laws governing elections and related matters.*

First Shedule:

> *(s) Provision of Civic Education and other related matters.*

H. RUSHWA NA MAADILI KATIKA SIASA NA UCHAGUZI

Sheria ya Uchaguzi Sura 343 imetaja adhabu za vitendo vya rushwa katika vifungu vya 94, 96 na 100. Hata hivyo maudhui ya vifungu hivyo ni ***kupambana na rushwa baada ya kutendeka na kwa atakayebainika***. Sheria haizuii vitendo vya rushwa katika uchaguzi. Madhara ya rushwa katika uchaguzi ni mengi miongoni mwake ni haya yafuatayo:

i. Kuwarubuni wapiga kura kuchagua bila utashi wao.
ii. Kumpa haki mtu asiyestahili (wasimamizi kumtangaza mgombea aliyeshindwa kuwa mshindi) na
iii. Udhalilishaji wa kingono (uteuzi wa viti maalumu wanawake).

Bahati mbaya kanuni za uchaguzi ambazo ndizo zilipaswa kutafsiri utekelezaji wa sheria za uchaguzi ziko kimya juu ya vitendo vya rushwa katika uchaguzi.

Tunafahamu kuwa makosa ya rushwa yako chini ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU/PCCB). Ni maoni yetu kuwa sheria ya uchaguzi badala ya kusubiri kupambana wakati makosa yametendeka, ingetaja uwepo wa TAKUKURU katika mchakato mzima wa uchaguzi ili kuzuia vitendo vya rushwa badala ya kusubiri vitokee ndipo vikabiliwe.

Ni maoni ya ACT Wazalendo kuwa makosa ya rushwa yaachwe kwa taasisi yenye mamlaka, weledi na uwezo kisheria kuyafanyia kazi. Uzoefu wa miaka ya nyuma unaonyesha kuwa TAKUKURU ilipokuwa sehemu ya uchaguzi kwa kusambaza

maafisa wake kufuatilia mchakato wa uchaguzi, hali ilikuwa shwari kwa kiasi fulani.

Kwa kufanya marekebiso hayo katika sheria ya uchaguzi Sura 343, tunaamini rushwa katika uchaguzi (kama kosa la jinai) itakabiliwa chini ya sheria ya TAKUKURU.

Utaratibu wa uandaaji maadili ya uchaguzi sio shirikishi. Maadili ya uchaguzi yanaandaliwa na Tume na Serikali. Ushirikishwaji wa wadau wa siasa ni wa kinadharia tu na hata maoni ya wadau hayazingatiwi ipasavyo.

Ni maoni ya ACT Wazalendo ni kuwa kifungu cha 124A cha Sheria ya Uchaguzi Sura 343 kiboreshwe kwa kuongeza kifungu kidogo cha 124A(2) ambacho kitaainisha utaratibu wa kuandaa maadili ya uchaguzi na kurekebisha kifungu kidogo (3) kuwa (4). Kifungu hicho kipya kisomeke ifuatavyo:

124A (2). The procedure for making the Electral Code of Conduct for Presidential, Parliamentary, Councillors and Harmlets elections shall be as prescribed here under:

a) *The Commission shall in not less than 60 days before the date publisised in the Gazzette for election, make notice to all political parties for submitting their proposals;*

b) *The Commission shall make compilation of the proporsal received and come up with the 1st draft;*

c) *The Commission shall in not less than 30 days before the date publisised in the Gazzette for election summon a*

consultative meeting with all stake holders for deliberations to enable the Commission to come up with the zero draft;

d) *The Commision shall shall in not less than 15 days before the date publisised in the Gazzette for election summon a second consultative meeting for endorsement.*

I. UHUSIANO WA SIASA NA MAWASILIANO KWA UMMA

Vyama vya siasa vipo kwa ajili ya kutoa sera na mwelekeo wa kisiasa nchini. Sera za vyama zinapaswa kufika kwa umma sio tu kwa ajili ya kuungwa mkono na kuongeza wanachama, lakini pia kukubalika na hatimaye kupigiwa kura katika uchaguzi (***legitimation***). Hata hivyo sio rahisi kuwafikia wananchi wengi. Nyenzo ya kufikisha ujumbe kwa umma ni kupitia vyombo vya habari.

Hata hivyo, uhusiano wa vyama vya siasa hususan vya upinzani umekuwa sio mzuri katika kipindi cha takriban miaka sita (6) iliyopita.

Ilifikia mahali chama cha upinzani kikitangaza kuitisha mkutano wa vyombo vya habari, waandishi wa habari kwanza wanataka kufahamu ajenda ili kuamua kuja au kutokuja. Lakini pia ilikuwa vigumu kwa vyombo vya habari kufanya mahojiano ya moja kwa moja na wanasiasa wa upinzani ili kujiepusha kuingia matatani na dola. Hata kama yalifanyika mahojiano, basi ilitolewa tahadhari kutoikosoa serikali vinginevyo yalizuiwa na wahariri yasirushwe. Sababu kubwa ilikuwa ni mabadiliko ya sheria na kanuni za maudhui ya habari ambayo kama ilivyofanyika kwa sheria ya vyama vya siasa, ilibinya uhuru wa vyombo vya habari katika kufanya kazi zake. Kwa kiwango fulani uandishi wa habari ulifanywa kuwa jinai. Hali hiyo ikiunganishwa na kuzuiwa kwa mikutano ya hadhara ilivifanya vyama vya siasa kukosa mawasiliano na umma.
Mapendekezo ya ACT Wazalendo ni kuruhusu mikutano ya hadhara kama ilivyoainishwa hapo juu na kuviacha vyombo vya habari vitekeleze wajibu wake (kwa kurekebisha sheria ya habari na kanuni za maudhui) ili kuwezesha uhusiano wa siasa na mawasiliano kwa umma.

MAONI NA MAPENDEKEZO YA ZIADA YA ACT WAZALENDO KUHUSIANA NA SHERIA ZA VYAMA VYA SIASA SURA 258 NA UCHAGUZI (NEC) SURA 343

Bila kuathiri maoni yetu tuliyowasilisha katika aya zilizotangulia hapo juu tunaamini kuwa suluhu ya matatizo/changamoto za vyama vya siasa na uchaguzi nchini ni ukamilishaji wa mchakato wa **KATIBA MPYA** na utungaji mpya/marekebisho makubwa ya Sheria ya Vyama vya Siasa sura 258 na Tume ya Taifa ya Uchaguzi sura 343. Kwa lengo hilo maoni ya ACT Wazalendo ni kama ifuatavyo:

(a) Sheria ya Vyama vya Siasa sura 258 (RE 2019)

1. **Tafsiri (Interpretation)**
   Kifungu cha (3) tafsiri ya neno "Registrar" irekebishwe na kusomeka:
   - ***"Registrar"*** *means the Registrar of Political Parties mentioned under section 4 and includes a deputy and an assistant registrar;*
   - ***"coalition"*** *means an alliance of two or more political parties formed for the purpose of pursuing a common goal and is governed by a written agreement deposited with the Registrar;*
   - **"Commission"** means the Independent Electoral Commission established under Article 74 of the Constitution;
   - **"Tribunal"** means the Political Parties Disputes Tribunal established under section 21F;

2. **Usajili wa vyama vya siasa**
   - Ufanywe na **Tume Huru ya Uchaguzi**.
   - Mafunzo ya elimu ya uraia (civic education) na kujiongezea uwezo (capacity building)

yanayoandaliwa na vyama vya siasa vyenyewe kutokana na mahitaji yake yasidhibitiwe na Msajili wa Vyama vya Siasa. Vifungu 4(5)(f) na 5A vinavyolenga udhibiti wa mafunzo yanayoandaliwa na vyama vya siasa vifutwe.

- Dhana ya ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuwa taasisi huru (***body corporate)*** inaondosha kinga ya kushitakiwa kwa msajili na mtumishi ndani ya ofisi yake. Kinga kwa maafisa wa vyama iondolewe ili kulinda uadilifu, nidhamu na uwajibikaji wao. Kifungu 5B(6) kifutwe.
- Masuala ya Muungano na usawa wa jinsia yazingatiwe (msajili na naibu wake watoke pande tofauti za Muungano na izingatiwe jinsia).

Kwa muktadha huo, sehemu ya II ya sheria inayohusiana na uanzishwaji wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa (**Establishment of the Office of the Registrar**) ifanyiwe marekebisho makubwa na kusomeka ifuatavyo:

4. Establishment of the Office of the Registrar

(1) There shall be established an office of the Registrar of Political Parties which shall be a body corporate with power to sue and be sued under the Commission.

(Appointment of the Registrar of Political Parties)

(2) There shall be employed by the Government Service Commisssion a Registrar of Political Parties who shall be a chief executive officer of the Office of the Registrar of Political Parties.

(3) There shall be a Deputy Registrar who shall be employed by the Government Service

Commisssion, resident of the opposite side of the union and with different gender to the Registrar.

(4) The Registrar shall be responsible for the registration of political parties in accordance with the provisions of this Act and shall perform any other functions as conferred by this Act.

(5) Without prejudice to subsection (4), the functions of the office of the Registrar shall be to;

a) *Register political parties in accordance with this Act and any other written law;*
b) *Supervise the administration and implementation of this Act;*
c) *Monitor intra-party elections and nomination process;*
d) *Disburse and monitor accountability of Government subventions to political parties which qualify under this Act;*
e) *Monitor income and expenditures of political parties and accountability of party resources;*
f) *Provide civic education regarding multiparty democracy, laws governed by the registrar and related matters;*
g) *Advise the Government on issues related to political parties and multiparty democracy;*
h) *Facilitate communication between political parties and the Government;*
i) *Undertake research on political parties, multiparty democracy and political parties financing;*
j) *Provide secretariat to the political parties' council and*
k) *Undertake any other functions conferred by this Act or the Commission's Act.*

(6) In the performance of functions under this Act, the Registrar shall from time to time consult the Commission.

(7) Appointment of assistant registrars and other officers

The Commission may appoint assistant registrars and such other officers in such numbers as may from time to time be required to carry out the purposes of this Act.

5. Sehemu IIA ya uanzishaji chama cha siasa ***(formation of a political party)***

- Kifungu cha 6A(5), suala la ***Mwenge wa Uhuru*** limewekwa mahali pasipotakiwa (misplaced) kwani halihusiani na uchaguzi wa viongozi/uteuzi wa wagombea wala uandaaji na utekelezaji wa sera za chama cha siasa. Vilevile kwa kuwa uanzishwaji wa chama umebainisha kuzingatia Katiba za nchi na sheria, masuala mengine yanayotajwa hayana sababu ya kurejerewa. Maneno hayo yaondolewe na kufanya marekebisho ili kifungu hicho kisomeke:

6A(5) A political party shall promote the union of the United Republic, the Zanzibar Revolution, inclusiveness, gender, participation of the people, democracy, good governance, in the-

(a) Formulation and implementation of its policies:

(b) Nomination of candidates for elections; and

(c) Election of its leaders.

- Kifungu cha 6B kinachohusiana na sifa za mwombaji usajili wa chama cha siasa ***(qualification of people applying for registration of a political party),*** umri wa mwombaji uwe sio chini ya miaka 21 kuendana na matakwa ya Sheria ya Uchaguzi Sura 343 kwa sababu ya kuweza kugombea uongozi wa kiserikali. kisomeke:

  6B(d) That person has attained or is above the age of twenty-one years;

- Kifungu 6C kuhusu masharti ya uanachama (***restrictions in party membership and participation in political parties activities).*** *Kifungu* 6C(1)(b) kirekebishwe miaka isomeke:

  b) Has attained or is above the age of eighteen years.

6. Sehemu ya III inayohusu usajili wa vyama vya siasa **(registration of political parties),** kifungu cha 8(7) kifanyiwe marekebisho ili kutamka bayana muda ambao Msajili wa Vyama vya Siasa atatakiwa kutoa usajili wa muda kudumu au majibu ya kukataa usajili kwa chama cha siasa kilichowasilisha maombi ya kusajiliwa. Kifungu hicho inapendekezwa kisomeke ifuatavyo:

(7) The Registrar shall register and issue a certificate of provisional registration or, as the case may be, a certificate of full registration to every political party which fulfill all the conditions for such registration ***within 45 calender days from the date of the application****.*

7. Kifungu 8E kuhusiana na vikosi vya ulinzi (***political parties not to form security group)*** kiangaliwe upya. Vyama vya siasa vina mali na viongozi wake

hawana ulinzi katika shughuli zao. Vilevile serikali (isipokuwa kwa chama kinachoongoza serikali) haijaweka utaratibu wa ulinzi. Suala la ulinzi wa viongozi na mali za vyama zinawekewa utaratibu gani kama vyama haviwezi kuwatumia vijana wake wa kujitolea, wenye mafunzo ya kujihami (ukakamavu) na wasio na silaha kulinda viongozi na mali za vyama? Kifungu hicho kirekebishwe kwa kuzingatia hukumu ya Mahakama ya Afrika Mashariki katika kesi ya Freeman Mbowe, Seif Sharrif Hamad na Hashim Rungwe dhidi ya serikali ilyobatilisha kifungu kicho. ACT Wazalendo inapendekeza kifungu hicho kisomeke:

> *8E. – A political party, a leader or member shall not recruit, deploy or form a militia or paramilitary* ***except party members' security groups meant to facilitate protection to its leaders and maintain security to the party properties.***

8. Sheria ya vyama vya siasa ifanyiwe marekebisho katika kifungu cha 4 kufanya elimu ya uraia kuwa miongoni mwa masuala muhimu ya kikatiba kwa vyama vya siasa. Marekebisho hayo yafanyike pia kwenye kiambatanisho cha kwanza (first schedule) na kusomeka ifuatavyo:

> *9(2)(g) It does not allow provision of civic education regarding multiparty democracy, laws governing elections and related matters.*

First Shedule:

> *(s) Provision of civic education and other related matters.*

9. Iongezwe fasili mpya 10(1)(g) kuhusu usajili wa kudumu (**conditions for full registration**) kulinda uwiano wa jinsia na kisomeke:

> *"10(1)(g) not less than 30% of the national leadership are women;*

Kisha yafanywe marekebisho ya mpangilio ili fasili (g) iwe (f) na kadhalika.

10. Sehemu ya IV inayohusu haki na fursa kwa chama cha siasa (**rights and privileges of registered political parties)** imekuwa ikitumiwa vibaya na Jeshi la Polisi kwa maelekezo au ushabiki wa CCM, kuzuia na hata kuvamia mikutano ya nje na ndani ya vyama vya siasa vya upinzani, kuanzisha vurugu, kuweka watu mahabusu, kusababisha majeruhi, vifo na kesi za kubambikiza. Vilevile vyama vya siasa havikupewa haki kisheria ya matumizi ya vyombo vya habari vya serikali na hivyo haki hiyo kuwa ya CCM pekee.

ACT Wazalendo inapendekeza kufutwa kwa kifungu cha 11(2) kinachotoa mamlaka ya matumizi ya vifungu vya 43 – 46 vya sheria ya Jeshi la Polisi (Police Force and Auxilliary Service Act Cap 322 of 1973) katika mchakato wa uitishwaji wa mikutano ya vyama vya siasa. Kifungu hicho kwa maudhui ya vifungu 43 – 46 vya sheria ya Jeshi la Polisi, ni kana kwamba taarifa ni ya kuomba kibali na kama kibali hakijatolewa basi kwa utashi wa Jeshi la Polisi, wakati wowote mkutano unaweza kuvunjwa hata kama utakuwa umeanza na unaendelea. Hayo ndiyo yamekuwa mazoea hususan kuanzia kipindi cha serikali ya awamu ya tano. Mapendekezo ni kukiandika upya kifungu cha 11(2) ili kisomeke ifuatavyo:

> ***11(2) Nothing in section 11(1)(a) shall be construed as applying for permission***

from the police officer inchage to hold meetings, but a notification for the protection and assistance of the security agencies for the purposes of facilitating peaceful and orderly meetings.

Ifahamike kuwa vifungu 43 – 46 vya Jeshi la Polisi vilitungwa kukidhi mahitaji ya mikutano na mikusanyiko mingine (maandamano, mikutano ya kidini n.k.) kwani wakati huo (1973) nchi ilikuwa na chama kimoja cha siasa ambacho kilikuwa tawala na hivyo Jeshi la Polisi halikuhusika na mikutano ya kisiasa. Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 1992 imevipa haki vyama vya siasa kufanya mikutano kwa kutoa taarifa polisi ili kupata ulinzi. Haiwezekani sheria ya vyama vya siasa ikatoa haki halafu, ndani yake kukawa na vifungu *(clause potestative)* vinavyoondoa haki hiyo.

11. Inapendekezwa kuongeza fasili(c) itakayofanya kuwa haki kwa vyombo vya habari vya serikali kutumiwa na vyama vyote na inapendekezwa fasili hiyo isomeke ifuatavyo:

    10(1)(c) to the provision by the state of fair opportunity to present the political party's programmes to the public by ensuring equitable access to the state owned media.

12. Pia kukifanyia marekebisho kifungu cha 11(8) ili kutoa muda ambao ndani yake afisa wa Jeshi la Polisi aliyepewa taarifa ya mkutano wa chama cha siasa atapaswa kujibu kuzuia mkutano usifanyike kama kuna pingamizi la kweli. Kifungu hicho kisomeke ifuatavyo:

    11(8) A stop order referred to under subsection (6) shall be made in writing ***within 12 hours after reception of notification from a political party,*** *and in such form as is able to easily disclose the*

reasons for its issuance and state whether or not the political party concerned may hold the meeting or procession at the venue or place at another time or date convenient to it in the same area and shall not be given except for the reasons described here under:

a) Coincidence of public meetings of two parties in tha same area and time,
b) Coincidence of the public meeting and government/community programmed activity,
c) State of emergency.

Kujibiwa ndani ya saa 12 kunalenga kukifanya chama kilichotoa taarifa kutoendelea na maandalizi na hivyo kuepusha kuingia gharama zaidi.

13. Kifungu cha 8E kinachohusu makundi ya ulinzi kwa vyama vya siasa kifutwe na kiandikwe upya kuzingatia uamuzi wa mahakama ya Afrika Mashariki ambayo ilitamka kinakinzana na mkataba wa Afrika Mashariki ambao Tanzania ni mwanachama na imeuridhia. Kifungu hicho inapendekezwa kisomeke ifuatavyo:

> *8E. – A political party, a leader or member shall not recruit, deploy or form a militia or paramilitary* ***except party members security groups meant to facilitate protection to its leadres and maintain security to the party properties.***

Ni maoni yetu kuwa marufuku iliyomo katika ibara ya 147 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) kuhusiana na makundi ya ulinzi inajitosheleza.

14. Kifungu cha 11A(3) kuhusu kushirikana vyama vya siasa (***coalition of political parties***) kirekebishwe

kwa kupunguza muda wa kuwasilisha mkataba kwa msajili na kisomeke ifuatavyo;

> - *11A(3) A coalition agreement entered into before a general election shall be submitted to the Registrar at **least 14 days** prior to the nomination of candidates to that General election.*

15. Maadam uanzishwaji na uendeshaji shughuli za kisiasa zimezuiliwa kwenye taasisi za elimu kifungu kidogo cha 12(5) kifutwe.

16. Kifungu cha 13A kinachoweka ulinzi kwa watoa taarifa (**Protection of informer and witness**) kifutwe kwani kwa kutowataka kutoa ushahidi mahakamani (vifungu vidogo 13A(2-4) kunaweka mwanya wa umbea na kutungwa uongo katika ofisi ya msajili wa vyama vya siasa jambo ambalo lina viashiria vya ofisi ya msajili kutumika kisiasa kuzua migogoro kwenye vyama. Hakuna sababu ya kuficha ushahidi kwa tuhuma dhidi ya chama kama ni za kweli. Wajibu wa kutoa ushahidi (*the burden of proof*) ni jukumu la mwenye kutuhumu chini ya sheria ya ushahidi (The Evidence Act of 1967) na uendeshaji wa kesi za makosa ya jinai na madai na sio aliyeambiwa (msajili).

17. Kifungu cha 16(3) kinachoainisha sifa za chama kustahiki ruzuku kiboreshwe kwa kuongeza fasili mpya tano (5) zinazoshajihisha vyama vyote vya siasa kushiriki uchaguzi, kuzingatia uwiano wa jinsia na kuwa na matumizi mazuri ya fedha za umma zitakazotolewa kama ruzuku. Kifungu hicho inapendekezwa kisomeke ifuatavyo:

> *"16(3) No party shall qualify for the grant to it of a subvention in accordance with this Act unless:-*

(h) It is a party which is fully registered and maintains conditions prescribed for full registration *under this Act,*

(i) Has been inspected by the Registrar of political parties,

(j) It has put up 5% of its candidates in the immediately preceding Civic Elections,

(b) It has, in the immediately preceding general and Local

Government election, had any of its candidates elected to be

a Member of Parliament or Member of a Local Government

Authority,

(k) *It has, participated in the immediately preceding general election and has attained at least 3% of the total valid votes for parliamentarians.*

(l) *It has, participated in the immediately preceding general election and has attained at least 1% of the total valid votes for councellors.*

(m) Not less than 30% of its national leaders are women,

(n) It has not attained either adverse or disclaimer opinion from the immediately preceding financial

statements audited by the Controller and Auditor General.

18. Kifungu cha 17(2) kinachohusu mgao wa ruzuku kiboreshwe kuwezesha vyama vyote vyenye usajili wa kudumu na vyenye kukidhi matakwa ya kifungu cha 16(3) kupata ruzuku ili kumudu gharama za utawala. Kifungu hicho inapendekezwa kisomeke ifuatavyo:

> *2(a)* ***ten*** *per centum of the funds shall be disbursed equally amongst qualifying parties on the basis of the conditions prescribed in sec. 16(3),*
>
> *(b)* ***forty*** *per centum of the funds shall be disbursed amongst qualifying parties on basis of the ratio of parliamentary seats;*
>
> ***(c) Twenty five*** *per centum of the funds shall be disbursed amongst qualifying parties on basis of the ratio of parliamentary valid votes*
>
> *(c)* ***Twenty five*** *per centum of the funds shall be disbursed amongst qualifying parties based on ratio of the councellors valid votes.*

19. Kifungu cha 18(3) kinachohusu kusitishwa ruzuku (**forfeit the right to any subsequent subvention**) kibainishe uwajibikaji wa vyama vya siasa kwa fedha za ruzuku. Fasili (3) iboreshe kuonyesha wajibu wa kutumia vizuri, kufunga hesabu na kupata hati safi. Kisomeke ifuatavyo:

- *18(3) Any party which fails or neglects to account for subventions subject to*

section 18A of this Act or ***attains adverse or disclaimer opinion*** *shall forfeit the right to any subsequent subvention due to the party in accordance with this Act.*

20. Aidha kifungu 18 kiongezewe angalizo (proviso) kwa ruzuku iliyositishwa kwa muda chini ya fasili 18(6) ili irejeshwe mara baada ya chama kurekebisha kosa sababishi. Angalizo liwekwe mara baada ya fasili (8) na lisomeke:-

    - *Provided that the grant of subvention suspended subject to subsection (6) should be reimbursed no sooner the party registers compliance (settlement) with the Act.*

21. Kiongewze kifungu kipya cha 18B kinachohusu ukaguzi wa fedha za ruzuku katika ofisi ya msajili wa vyama vya siasa ambazo ni sehemu ya ruzuku ya serikali ili kuongeza uwajibikaji kwa fedha za umma. Fasili hiyo isomeke:

    18B: Accounts and audit of the Office of Registrar

    - *(1) The Office of Registrar of Political Parties shall keep proper books of account of the income, expenditure and assets of the Office.*

      (2) Within a period of three months after the end of a financial year, the Office of Registrar of Political Parties shall submit to the Auditor-General, the accounts of the Office together with—

(a) a statement of the income and expenditure of the Office during that year; and

(b) a statement of the assets and liabilities of the Office during that year.

3) All accounts kept under this Act shall be audited by the Auditor-General at least once in every financial year.

22. Kifungu cha 19(1) kuhusiana na kufutiwa usajili chama cha siasa (***suspend or* cancel registration**) kirekebishwe kulazimisha vyama vya siasa kushiriki chaguzi za serikali za mitaa na uchaguzi mkuu ili kuakisi lengo la kusajiliwa kwavyo (kutafuta kuongoza dola) na kuleta ushindani. Chama kisichoshiriki au kikishiriki kikashindwa kukidhi matakwa ya sheria kufutwe. Jambo hilo litaongeza umakini (seriousness) katika unzishwaji na uendeshaji wa vyama vya siasa na kupunguza utitiri wa vyama dhaifu vibaraka ***(puppet parties).*** Kifungu hicho sasa kisomeke ifuatavyo:-

- ***19. Power of Registrar to suspend or cancel registration***

  (1)Subject to subsection (2) the Registrar may refer to the Tribunal the suspention or cancelletion of registration of any political party which has contravened any of the provisions of this Act or which has otherwise ceased to qualify for registration under this Act or has failed to put 5% of candidates in the immediately preceding general or local government election or has participated in any general election and failed to

attain at least 0.3% of all the valid votes cast in the parliamentary or House of Reprentative election for all the qualifying parties.

23. Viongozi wakuu wa Baraza la Vyama vya Siasa (Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti) wasichaguliwe bali wapatikane kwa mzunguko (revolving) kutoka chama kimoja kwenda kingine. Kifungu cha 21 B(3) kisomeke;

    - *"21B(3)The Chairman and the Vice Chairman of the Council shall be revolving amongst political parties members of the Council."*

24. Kifungu cha 21 C(1) kifanyiwe marekebisho katika fasili (a) na kuongezwa fasili tatu mpya (f), (g) na (h) zinazosomeka ifuatavyo:-

    - *21C(1) (a) Deliberate on the disputes arising amongst political Parties and advise the registrar accordingly before referring them to the* ***Political Parties Dispute Tribunal****.*

      (f) Hold consultational meeting(s) in each financial year with the Minister responsible for matters relating to political parties or the Prime Minister to deliberate on matters of national interest with reference to political Parties or political stuation;

      (g) Ensure respect and adherence to to the Constitution, Political Parties Act and other laws of the land amongst Political Parties and the Government;

h) To provide a platform for dialogue between the Registrar, Commission and political parties.

25. Kuanzisha Baraza la Usuluhishi wa Migogoro ya vyama vya siasa ***(Establishment of the Political Parties Dispute Tribunal)***. *Kuongeza vifungu vipya 21(F-J) vinavyosomeka ifuatavyo:-*

- **21F: Establishment of the *Political Parties Dispute Tribunal***

  (1) There shall be established a Tribunal known as ***The Political Parties Dispute Tribunal*** *which shall be responsible for handling disputes arising amongst political Parties for redress in order to maintain peace and harmony in political activities.*

  (2) The minister after consultation with the Chief Justice may make regulations *prescribing the manner the* ***Political Parties Dispute Tribunal*** *should carry out its duties under this Act* and removing any difficulties occasioned by the coming into operation of the Tribunal*;*

  (3) Without prejudice to subsection (1), the final say of the measures for non compliance of the Act and its regulations shall be vested to the Tribunal.

  (4) The Tribunal shall consist of the following members, appointed by the Judicial Service Commission:-

  (a) A Chairperson who shall be a person qualified to be appointed a judge of the High Court; and

(b) Six other members, three of whom shall be Advocates of the High Court of at least seven years standing and three other wisdomed professionals (public spirited citizens) without standing governance, administrative, social, political, economic and other record.

(c) The Chairperson and members of the Tribunal shall serve on part-time basis.

(d) The Chairperson and the members shall hold office for a non-renewable term of five years.

(e) A person shall not be qualified to be appointed as a member of the Tribunal if that person is a member of the public service or takes an active part in the activities of a political party.

(f) A person shall not assume office unless he has taken and subscribed the oath of allegiance and such other oath as may be prescribed by regulations made by the Chief Justice under the Act.

- **21G: Determination of Disputes**

(1) The Tribunal shall determine:-

(a) Disputes between the members of a political;

(b) Disputes between a member of a political party and a political party;

(c) Disputes between political parties;

(d) Disputes between the registrar and a political party or political parties;

e) Disputes between coalition partners;

(f) Appeals from decisions of the Registrar under this Act; and

(g) Punishments and penalities refered to by the registrar after due deligence.

(2) Notwithstanding subsection (1), the Tribunal shall not hear or determine a dispute under paragraphs (a), (b), (c) or (e) unless the dispute has been heard and determined by the internal political party dispute resolution mechanisms.

- **21H: Period for determination of disputes**

(1) The Tribunal shall determine any dispute before it expeditiously, but in any case shall determine a dispute within a period of three months from the date the dispute is lodged.

(2) An Appeal shall lie from the decision of the Tribunal to the High Court on points of law and facts and on points of law to the Court of Appeal.

(3) A decision of the Tribunal shall be enforced in the same manner as a decision of a Magistrates Court.

(4) The Chief Justice, in consultation with the Tribunal may, prescribe regulations for determination of disputes under this section.

(5) The Tribunal shall apply the rules of evidence and procedure under the Evidence Act (No.6 of 1967) and the Civil Procedure Act (Cap. 33), with the necessary modifications, while ensuring that its proceedings do not give undue regard to procedural technicalities

- **21I: Staff of the Tribunal**

  The Judicial Service Commission shall appoint the Secretary and such other staff of the Tribunal necessary for the proper functioning of the Tribunal.

- **21J: Expenses of the Tribunal**

  The remuneration of the members, staff of the Tribunal and the expenses of theTribunal shall be paid out of monies allocated by the National Assembly to the Judiciary Fund as shall be determined by the Judicial Service Commission on the recommendation of the Salaries and Remuneration Commission.

(b) Sheria za uchaguzi (NEC & ZEC)

Bila kuathiri maoni na mapendekezo yaliyotangulia hapo juu, mtazamo wetu kwa kipindi cha muda mrefu juu ya **MASUALA YANAYOHUSU UCHAGUZI,** ACT Wazalendo tunaona kuna haja kubwa ya kuzingatia mapendekezo ya Tume ya Jaji Nyalali ya kuandikwa upya au kufanyiwa marekebisho makubwa Sheria ya Uchaguzi ya Taifa (National Elections Act Sura 343) na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar (Zanzibar Elections Act) ili kuzifanya ziwe na miundo inayozingatia matakwa na misingi ya demokrasia ya vyama vingi. Kwa Tume Huru ya Uchaguzi ya Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania (Independent Electoral Commission) inapendekezwa sheria ya uchaguzi (NEC) iwe na muundo ufuatao:

TUME HURU YA UCHAGUZI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

Tume ya Uchaguzi ni zao la Katiba na Sheria. ACT Wazalendo tunapendekeza kuandikwa upya kwa Sheria ya Uchaguzi na Kanuni zake ili kupata Tume Huru ya Uchaguzi. Tunapendekeza kuwa Tume Huru ya Uchaguzi iwe na uwezo wa kuajiri Wasimamizi wa Uchaguzi katika ngazi zote na kuondokana kabisa na Mfumo wa sasa wa makada wa Chama tawala kuwa Wasimamizi wa Uchaguzi. ACT Wazalendo tunapendekeza kufanya marekebisho ya ibara ya 74(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili itamke bayana maneno “TUME HURU YA UCHAGUZI”. Pamoja na mapendekezo mazuri ya Rasimu ya Tume ya Jaji Warioba; ambayo yana msingi wa kuwa maoni ya wananchi wenyewe, tunashauri ipitiwe upya na Kamati ya Wataalamu wenye maadili mema, ili kufanya marekebisho mengine yatakayoakisi mazingira ya sasa ya kisiasa na kijamii nchini.

MUUNDO WA TUME HURU YA UCHAGUZI

Muundo wa Tume ya Uchaguzi kwa mujibu wa ibara ya 74(1–2) ya Katiba na kifungu cha 4(1) cha sheria ya Uchaguzi Sura 343, unajumuisha;

Wafanyakazi wa aina tatu (3):

a) Kundi la kwanza ni wafanyakazi wanaoteuliwa na Rais (Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Mkurugenzi wa Tume ya Uchaguzi na wajumbe wengine watano (mmoja kutoka Chama cha Mawakili Tanganyika na wajumbe wengine wanne ambao wana uzoefu wa kuasimamia uchaguzi wa wabunge au sifa nyingine ambazo Rais ataona inafaa kuwateua kuwa wajumbe wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi);

b) Kundi la pili ni wafanyakazi wa kudumu na;

c) Kundi la tatu ni wafanyakazi wa muda wanaoteuliwa muda wa uchaguzi (wasimamizi wa Uchaguzi ambao ni wakurugenzi wa Halmashauri za Jiji, Miji na Wilaya) kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi.

Muundo huu unampa madaraka Rais kumuondoa mjumbe yoyote katika Tume ya uchaguzi kutokana na sababu tatu zifuatazo:-

a) Kama kamaliza muda wa miaka mitano;
b) Kwa kushindwa kutimiza majukumu yake kwa sababu ya ugonjwa au;
c) Sababu nyingine yoyote ama kwa kosa la utovu wa nidhamu.

Hali hiyo inawafanya wajumbe wa Tume kufanya kazi kwa kutojiamini/woga na muda mwingi kufanya kazi zao kwa maelekezo ya mamlaka ya uteuzi, jambo linaloiondolea Tume uhuru. ACT Wazalendo inapendekeza kuifanyia marekebisho makubwa; vinginevyo, kuiandika upya sheria ya uchaguzi ili kuwa na muundo mpya unaoakisi Tume Huru ya Uchaguzi kama ifuatavyo:

1) MUUNDO WA TUME HURU YA UCHAGUZI (Sheria mpya ya uchaguzi)

a) Sheria mpya ya Uchaguzi (National Elections Act 2022) iweke utaratibu kuwa Watanzania wanaotaka kuwa Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi waombe kazi kufuatia tangazo la wazi kwa umma.

b) Sheria mpya ya Uchaguzi ianzishe Kamati Maalumu ya Uteuzi wa Mwenyekiti,

Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi.

c) Kamati ya Uteuzi ifanye usaili (interview) kwa uwazi kwa waombaji wote na kuchuja majina na kupendekeza majina matatu (3) kwa Rais kwa ajili ya uteuzi. Mara baada ya wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi kupatikana wataajiri Mkurugenzi wa Uchaguzi kwa kutangaza, kisha kufanyiwa usaili wa wazi na Kamati Maalumu ya Uteuzi ambayo itapendekeza majina matatu (3) kwa Rais kwa ajili ya uteuzi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi. Rais hataruhusiwa kurejesha jina la Mkurugenzi aliyependekezwa na Kamati maalumu baada ya kumfanyia usaili.

d) Kamati Maalumu ya Uteuzi

e) Tume ipewe mamlaka ya kuajiri watu wa muda watakaofanya kazi katika kipindi cha uchaguzi. Wakurugenzi hawataruhusiwa kuwa wafanyakazi wa muda wa tume.

f) Kutakuwa na sifa maalumu za Mwenyekiti na wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi ili kuhakikisha wanakuwa watu wenye weledi na hawaegemei upande wowote.

2) MUUNDO WA KAMATI MAALUMU YA UTEUZI WA WAJUMBE WA TUME HURU YA UCHAGUZI

Inapendekezwa kuwe na Kamati Maalumu ya Uteuzi (Selection Panel) wa wajumbe wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi ambayo muundo wake na upatikanaji wa wajumbe utatokana na makubaliano ya Mkutano wa Majadiliano ya Kitaifa ***(National Consultative Conference).*** Mapendekezo hayo yanazingatia ukweli kwamba, utaratibu unaotumika katika nchi nyingine hautakuwa na tija kwa Tanzania mpaka suala la Katiba

Mpya liwe limekamilika. Mapendekezo yetu ya utaratibu wa kutumika katika kipindi cha sasa cha mpito kuelekea Katiba Mpya tumeueleza kwenye ukurasa wa 26-27 wa kitabu hiki.

Kwa upande mwingine, utaratibu wa muundo wa kudumu wa Kamati ya Uteuzi tunaoupendekeza uwemo kwenye Katiba Mpya (ambayo pia itakuwa imeweka misingi ya taasisi nyingine za nchi kuwa huru) uwe kama ifuatavyo;-

e) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano kama Mwenyekiti,
f) Jaji Mkuu wa Zanzibar kama Makamu wa Mwenyekiti,
g) Rais wa Tanganyika Law Society,
h) Rais wa Zanzibar Law Society,
i) Watu wawili kutoka Chama cha Wanasheria Wanawake; mmoja kutoka Tanzania Bara na mwingine kutoka Zanzibar,
j) Watu wawili kutoka Taasisi za masuala ya Wanawake; mmoja kutoka Tanzania Bara na mwingine kutoka Zanzibar,
k) Watu wawili kutoka Asasi za Kitaifa za masuala ya Sheria na Haki za Binaadamu, mmoja kutoka Tanzania Bara na mwingine kutoka Zanzibar.

3) SIFA MAALUMU ZA MWENYEKITI NA MAKAMU MWENYEKITI WA TUME HURU YA UCHAGUZI

a) Awe ni raia wa kuzaliwa na angalau mmoja kati ya wazazi wake ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano;

b) Awe ni mtu aliyewahi kushika nafasi ya madaraka ya Jaji wa Mahakama ya Juu, Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu na ameshika nafasi ya madaraka hayo kwa kipindi kisichopungua miaka

mitano au awe ni wakili ambaye amefanya shughuli za kiwakili kwa miaka kumi;

c) Awe ni mwaminifu, mwadilifu na mwenye mwenendo usiotiliwa shaka na jamii;

d) Awe ni mtu ambaye hajawahi kushika nafasi ya madaraka ya juu katika chama cha siasa; na

e) Awe mtu ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai.

4) SIFA MAALUMU ZA MKURUGENZI WA TUME HURU YA UCHAGUZI

a) Awe ni raia wa kuzaliwa na angalau mmoja kati ya wazazi wake ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano;

b) Awe ni mtu mwaminifu, mwadilifu, na mwenye mwenendo usiotiliwa shaka na jamii;

c) Awe ni mtu ambaye hajawahi kushika nafasi ya madaraka ya juu katika chama cha siasa;

d) Awe na shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa kwa mujibu wa sheria;

e) Awe na uzoefu wa kutosha wa kusimamia uchaguzi wa wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

f) Awe ni mtu ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai.

5) SIFA MAALUMU ZA WAJUMBE WA TUME HURU YA UCHAGUZI

a) Awe ni raia wa kuzaliwa na angalau mmoja kati ya wazazi wake ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano;

b) Awe ni mtu mwaminifu, mwadilifu, na mwenye mwenendo usiotiliwa shaka na jamii;

c) Awe ni mtu ambaye hajawahi kushika nafasi ya madaraka ya juu katika chama cha siasa;

d) Awe na shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa kwa mujibu wa sheria;

e) Awe ni mtu ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai.

6) MUDA WA MJUMBE WA TUME KUSHIKA MADARAKA

a) Mjumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi atashika nafasi ya madaraka kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja cha miaka mitano.

b) Mtu atakoma kuwa mjumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi endapo litatokea tukio lolote kati ya matukio yafuatayo:-

i. Kujiuzulu;

ii. Kutokuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya maradhi;

iii. Kukiuka kanuni za Maadili ya Uongozi wa Umma;

iv. Kutiwa hatiani kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifungo gerezani kwa muda unaozidi siku saba;

v. Kupoteza sifa ya kuteuliwa kuwa mjumbe; au

vi. Kufariki dunia.

c) Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu ya Tume, kutakuwa na kanuni za maadili kama zitakavyoainishwa na sheria.

d) Endapo suala la kumuondoa Mjumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi kwa kukiuka kanuni za maadili litajitokeza, Rais atateua Kamati itakayoundwa na:

i. Jaji wa Mahakama Kuu au Rufani ambaye atakuwa Mwenyekiti;

ii. Mjumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji;

iii. Mawakili wawili, mmoja kutoka Tanzania Bara na mmoja kutoka Zanzibar watakaopendekezwa na Chama cha Wanasheria Tanganyika na Chama cha Wanasheria Zanzibar;

iv. Mtu mmoja kutoka Asasi ya Kitaifa ya masuala ya Sheria na Haki za Binadamu Tanzania Bara au Zanzibar.

e) Endapo, baada ya uchunguzi, Kamati itapendekeza kuwa mjumbe huyo

aondolewe madarakani, Rais atamuondoa mjumbe huyo madarakani na endapo;

f) Kamati itapendekeza kuwa mjumbe huyo asiondolewe, suala la kumuondoa mjumbe huyo litakoma,

g) Kamati itaweka utaratibu wa kufanya uchunguzi.

7) UTEUZI NA RUFAA ZA WAGOMBEA

a) Mgombea asienguliwe kwa ajili ya makosa madogo madogo (minors or topografical erros) kwenye kujaza fomu na ni wajibu wa Tume kuhakisha inamsaidia mgombea kurekebisha makosa hayo.

b) Mgombea aliyekatiwa rufaa asiendelee kufanya kampeni mpaka Tume itoe uamuzi ili kupunguza pingamizi zisizo na tija zaidi kama njama za kumchelewesha mgombea kufanya kampeni.

8) KAMPENI

Kusiwe na kuingilia kampeni za uchaguzi bila sababu za msingi (unreasonable interference) kwa mgombea kipindi cha kampeni kunakofanywa na vyombo vya polisi kama vile kukamatwa kwa mgombea na kuswekwa rumande (unreasonable arrest).

9) GHARAMA ZA UCHAGUZI

a) Kuwepo kwa ruzuku ya uchaguzi kwa wagombea ili kuleta uswa kwa wagombea kuweza kufanya kampeni na pia Tume igharamie ghrama za msingi za uchaguzi kama vile kulipa mawakala.

b) Kupunguza gharama za kufungua kesi za uchaguzi kwani sheria ya sasa ya uchaguzi inataka mtu alipe shilling milioni tano kwa mshitakiwa mmoja kupinga matokeo ya uchaguzi wa mbunge.

10) MATOKEO YA UCHAGUZI

Kuwepo na kifungu cha sheria kinachoruhusu matokeo ya uchaguzi wa Rais kupingwa mahakamani.

NB: Sehemu zote zilizoandikwa kwa maandishi mazito (bolded) ni kuonyesha msisitizo au mabadiliko yanayopendekezwa na ACT Wazalendo

ACT WAZALENDO; TAIFA KWANZA LEO NA KESHO

ACT
WAZALENDO